

UNYAKUO

 Tawi hili hapa Yu—Yuma, ni heshima kubwa kupata mwaliko huu wa kurudi tena. Tulikuwa na wakati wa furaha sana, safari ya mwisho tulipokuwa hapa. Na halafu niana—ninapofahamu nilikuwa nirudi tena, ilinifanya nijisikie vizuri sana, kusikia shuhuda hizo na maneno haya ya kupendeza kutoka kwa watu, na kwa namna fulani inakutia moyo kidogo.

² Billy aliniambia ya kwamba yule ndugu kutoka Las Vegas, aliyetaka mkutano kule kwenye lile tawi, nimwone mara baada ya ibada kwisha hapa. Tuna wakati, yeye anasema, kwamba tunaweza kupitia, moja kwa moja katika Januari, kabla ya ule mkutano wa Phoenix, unaona, kuja—kuja Las Vegas. Na kwa hiyo sikuzote tulitaka kwenda kule.

Ninaamini Ndugu Art Wilson alikuwa akikaa kule, zamani sana, ama huenda akawa angali yuko kule. Naye ali—aliniomba nije huku, yeye na Dada Wilson. Sikupata nafasi, kwa hiyo labda huu utakuwa ndio wakati ambao ningeweza kuja.

³ Hebu tu mwoneni Billy Paul ama Ndugu Roy Borders. Nafikiri yuko hapa mahali fulani. Mtu fulani alisema Ndugu Roy alikuwa humu. Ndugu Pearry, Lee, ama ye yote wao, wataweza kuwaambia. Watupangie tu tarehe za sisi kuja.

⁴ Sasa, niliona wahudumu wengi hapa, hivi punde, ambapo nina furaha sana kukutana na ndugu zangu. Laiti ningalikuwa na wakati, kwenda nyumbani pamoja nanyi, maana ninajua mna mpishi bora sana aliyeko nchini. Hilo ni sawa.

⁵ Na sasa, Ndugu Pearry kweli ana mbili, usiku wa leo, dhidi yake. Ana alama mbili dhidi yake sasa. Mojawapo, ni kukata maikrofoni ile, kule. Ambapo, ume—umepatikana na hatia ya jambo hilo, Ndugu Pearry. Sidhani kwa kweli ulikuwa na hatia. Bali ulininii. . . Mtu fulani alikuwa akitaka kuzungumza. Hilo lilikuwa ni zuri.

⁶ Na kwa hiyo basi, tena, yeye alitoka nje pale na alikuwa akizungumza. Akasema, “Aisee!” Yeye anamwambia Ndugu Collins ama baadhi yao. Kasema, “Chakula cha jioni kilikuwa ni kizuri. Lakini,” kasema, “ninawaambia,” kasema, “mtu huyo hana budi kuwa ni Mhispaniola ama cho chote kile, ama Mmeksiko. Hiyo ilikuwa ni pilipili kali sana niliyopata kuonja.” Akiendelea namna hiyo; naye alikuwa akizungumza na mpishi mkuu.

Akasema, “Mimi ndiye mpishi mkuu.”

⁷ Hiyo ni Texas, kwenu. Tutamnyoosha, hapa Arizona, baada ya muda kidogo, (sivyo?), kama akikaa karibu na sisi.

⁸ Ni vizuri sana kuwapo hapa! Nami nafikiri hayo hayaelekei kama ni utani, bali ni ucheshi. Ambapo Bwana Mwenyewe alikuwa na tabia ya ucheshi, mwajua. Alisema, “‘Herode,’ nendeni mkamwambie yule mbweha, unaona, ‘leo ninatoa—natoa pepo, kesho nakamilika.’” Kwa hiyo, Yeye alikuwa na ucheshi. Vema, huo hautatudhuru, sidhani, mara moja moja.

⁹ Na sasa muda umeenda kidogo. Na, kwa kawaida, mi—mimi ninahubiri kwa kama saa nne. Kwa hiyo jambo hili, kwa kuwa ninajua heshima ya ndugu huyu na dada hapa, tawi hili, tutafupisha hayo sana, usiku wa leo. Na ninii tu... nilimwambia Terry, nikasema...

Yeye alisema, “Ni nini... Je! tuweke kanda ya masaa mawili?”

¹⁰ Nikasema, “La, Terry. Hii ni dhi—dhifa.” Nikasema, “Kama tu dakika thelathini ama arobaini, nitazungumza na watu juu ya jambo fulani.” Kwamba, ningejaribu, hata hivyo, kila wakati, nikijua jambo hilo.

¹¹ Nilipokuwa mvulana mdogo, watu walikuwa wakija kusikiliza kwa sababu nilikuwa mhubiri mvulana, kijana mdogo tu, mvulana. Nao wangesema, “Vema, Billy Branham, unajua, yeye ni mtoto tu, kamwe hakupitia shuleni, wala hana elimu.” Nao wangekuja kusikiliza maneno yangu yasiyo ya ufasaha, Kiingereza changu cha Kentucky, na—na kwa hiyo wao... “ii zangu, na iki, na ote na pepa zangu.”

Ni kama mmoja wa mikutano hiyo hapa si muda mrefu uliopita, wakasema, “Sote tutasimama na kuimba wimbo wa taifa.”

¹² Nilisimama na kusema “Napenda masikani yangu huko mbali Kentucky.” Hilo ndilo taifa pekee nililojua habari zake, kwa hiyo huo ulikuwa ndio wimbo wa taifa, niuavyo mimi.

¹³ Kwa hiyo sasa, baada ya kupata umri zaidi, hata hivyo, vema, sisi, anaingia, huna budi uwe na kitu fulani zaidi ya hicho. Unaona? Tutachukua... Paulo alisema, “Nilipokuwa mtoto, nilinena kama mtoto na kuwaza kama mtoto. Unatenda kama mtoto.” Bali unapokua zaidi, ndipo unaanza, kutoka katika kupiga hatua zako kadha za kwanza, na kuyumbayumba na kuanguka, kisha unainuka na kujaribu tena. Halafu wewe, baada ya kitambo kidogo, unafikia ambapo unaweza kutembea sawa. Na hilo ndilo linalotupasa kufanya, kama askari wa msalaba. Sasa wakati umewadia wa kutembea sawa, moja kwa moja kupitia kwenye hiyo barabara kuu ya kwenda katika Utukufu.

¹⁴ Ninaamini ya kwamba tunaishi katika matukio ya mwisho ya historia ya ulimwengu huu. Hakika ninaamini ya kwamba Kuja kwa Bwana kumekaribia, labda, kuliko tunavyodhanika. Kwa hiyo sasa, kwa yapata tu dakika thelathini za muda wenu, ama cho chote kile, ningetaka kuwakumbusha Andiko ambalo

ningetaka kutumia kwa ajili ya somo, na—na kurejea kwa mengine zaidi hapa.

Nikiwa nimeketi nyumbani, hivi majuzi, nilikuwa nikiwazia juu ya wazo hili. Ndipo nikawazia, “Vema, sijui, nikizungumza kutoka kwenye Maandiko haya yote. Nitachukua tu sehemu Yake, na kwa ajili tu ya ibada hizo ndogo tu kama tutakazokuwa nazo usiku wa leo.” Ninataka kusema jambo moja, wakati mnafungua Zaburi. Kifungu cha—cha 1, Zaburi 27, ninataka vifungu vya kwanza vitano, kusoma.

¹⁵ Ningetaka kusema jambo hili, kuhusu matawi haya ya wafanyabiashara ya Wafanyabiashara wa wa Full Gospel.

Ndugu yangu Pearry alikuwa akizungumza kuhusu vitabu, na kadhalika, na vitabu vipya walivyo navyo. Ni wangapi wanaokumbuka wakati tulipokuwa na kanda, na nikahubiri hapa Phoenix, katika mmojawapo wa ile mikutano, kuhusu *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Sasa, huo ulikuwa ndio mwanzo wa kitabu hicho, unaona, wakati ninii—jambo hili lilipotukia.

¹⁶ Kuna kuthibitishwa kwingi sana kwa mambo ya kiroho ya Neno la Mungu lililoandikwa, la wakati huu, lazima kitu fulani kinatukaribia sasa. Sisi tunaninii tu. . . Ni dhahiri mno. Mambo ambayo ninyi. . . Lingekuwa ni jambo la kushangaza sana, kwako, kukufahamisha yale ambayo yanatukia hasa. Wengi wenu, wageni, labda, mnawasikia watu hawa wakisimama na kufanya—kutoa matamshi haya, kuhusu, “Ujumbe wa wakati huu,” na kadhalika. Kile wanachomaanisha, ni ile ahadi ya Mungu ya wakati huu, ambayo aliahidi yale Yeye angefanya. Nasi tunamwona akithibitisha Kimaandiko barabara kabisa yale aliyosema angefanya, namna hiyo hiyo. Yalitabiriwa, yanatimia kikamilifu kabisa, kila wakati, kwa maana ni Mungu anayesema jambo hilo.

¹⁷ Kama mtu fulani, sijali yeye alikuwa ni nani, angejaribu kufanya ubashiri wa namna hiyo, kuna nafasi moja katika milioni kumi. Kama mtu alikwambia jambo *fulani* lingetukia, linge—lingetukia *wakati* fulani; moja katika milioni kumi. Na halafu *mahali* lingetukia, pangukuwa na kama nafasi moja kutoka katika milioni mia moja.

Na tena, *wakati* lingetukia, inaendelea na kuendelea, na *jinsi* litakavyotukia, na *vile* litakavyotukia, na kadhalika, haiwezi kukisiwa. Tunapoliona likiwa kakamilifu hivi, kila mara na kila wakati, basi ni Mungu.

Ndipo tunarudi moja kwa moja kwenye Maandiko. Linaweza kuonekana ni la kigeni kwetu. Lakini tunageuka moja kwa moja kwenye Maandiko, bila hata ya kujua tuangalie wapi, ndipo Roho Mtakatifu analeta na kuliunganisha Neno lote pamoja, linafanya picha hapo ya kutuonyesha saa tunayoishi. Tunabadilisha vipindi vya wakati.

18 Tuko—tuko kwenye kona. Ni rahisi wakati mtu anapokata kona, ya fundi mwashi wa matofali, anapokata kona. Huanzia, kila mtu anaweka matofali moja kwa moja katika safu ile ile, kama vile madhehebu fulani yanavyoanza, na kuanza kufingirika kwenye safu, hilo ni sawa. Lakini, unapofikia kona hizo, ambapo inakubidi kurudi upande huo mwingine!

Sasa, Mungu hajengi ukuta. Anajenga nyumba, unaona, na kuna mikato mingi na kona nyingi ambazo amebashiri hapa katika Biblia. Na hiyo mikato, mtu ye yote angeweza kujaribu kupiga kona, lakini haina budi iwe ni kulingana na mchoro. Kama siyo, itabidi ibomolewe tena.

19 Kwa hiyo tu—tunamtukuza Mungu kwa wema Wake na ushirika wenu ninyi watu, na milango iliyofunguliwa ambayo Bwana ametupa, na kupitia kwa hawa Wafanyabiashara. Daima nimeshikilia ya kwamba si—sikuamini katika...ninaamini katika watu katika madhehebu. Bali sina wakati mwingi wa kuyaonya madhehebu, kwa maana kila moja hujizungushia ukuta.

20 Na—na ni kama tu ninii, ninaamini ni ule msemu mdogo Ndugu David, kuhusu wakati alipokuwa akifuga bata wachache, akasema mto ulifurika. Ndipo na kila bata, wajua, walitaka ushirika wao kwa wao, wasingeweza kufanya jambo hilo kwa maana wote walikuwa wamezungushiwa ukuta. Lakini wakati maji yalipofurika sana, yaliwaelesha tu hao bata wakatoka kwenye hicho kizimba.

Kwa hiyo na—nafikiri hiyo ndiyo njia ya kufanya jambo hilo. Ni maji yanafurika, mnaona, nasi tunaweza kutoka kwenye kizimba na—na kufanya ushirika mmoja kwa mwingine, unajua, tuwe na upendo halisi wa Kristo mioyoni mwetu.

21 Na shirika hili la Wafanyabiashara wa Full Gospel limekuwa oasisi kwangu. Kwa maana, mara nyingi...nina ndugu, ndugu wazuri katika, nadhani, kila madhehebu niliyowahi kukutana nayo: Wapresbiteri, Walutheri, Wabaptisti, Wapentekoste, ninii—namna zote mbalimbali za Kipentekoste, Kanisa la Mungu, na Wanazarayo, Wapilgrim Holiness. Ndugu wazuri, kila mahali. Lakini, mara nyingi, hawawezi kuniruhusu nikae katika kundi lao, kwa sababu, unaona, si kwamba hawaamini huu, lakini, unaona, ungewakatilia mbali na madahehebu yao. Na unapofanya hivyo, bila shaka, hilo—hilo linasababisha jambo hilo.

22 Hapa si muda mrefu uliopita, kulikuwako na ndugu wa Kimethodisti aliyenijia, sitataja jina lake. Mtu mzuri. Alikuwa akiandika tasnifu juu ya Uponyaji wa Kiungu, naye akanijia tupate ku—kuzungumza. Tuliketi tukazungumza kidogo. Akasema, “Neno tulilo nalo tu dhidi yako, wewe daima unashikamana wakati wote na hao Wapentekoste.”

Nikasema, “Basi, hebu kanisa la Methodisti liudhamini. Nitakuja.”

Hilo lilikuwa ni kitu kingine. Unaona? A—akasema, “Vema, bila shaka, mi—mimi si kansa la Methodisti. Mimi ni wao tu.”

²³ Nikasema, “Hivyo ndivyo ilivyo. Unaona? Hao ndio, Wapentekoste, ndio wanaofungua milango yao. Unaona? Hao ndio ninaoweza kuwafikia. Na wote watakaofungua, mbona, tuko tayari kuingia.”

Kama vile Yeye alivyosema katika Ufunuo, sura ya 3, alisema, “Nasimama mlangoni na kubisha. Kama mtu ye yote akifungua mlango, nitaingia na nitakula.” Na huyo alikuwa ni Yesu. Sisi sote tuajua huyo alikuwa ni Kristo, Naye ni Neno. Hiyo ni kweli. Yeye ni Neno.

²⁴ Na kwa hiyo shirika la Wafanyabiashara wa Ijili Yote limekuwa ni oasisi ambapo tunaweza kukusanyika pamoja. Hakuna makanisa yanayolidhamini. Hao wote, kwa jumla, ni—ni watu walio nje ya makanisa, nasi tunakusanyika na kushiriki, ulimwenguni kote, kila mahali.

²⁵ Nami nimesaidia kuanzisha matawi mengi, mengi sana kote ulimwenguni, ya Wafanyi Biashara wa Full Gospel. Ninashukuru kwa ajili ya nafasi hiyo niliyopewa. Huko, Wafanyabiashara wataidhamini. Halafu, makanisa yote, wa—wanataka kuja, hata hivyo.

Lakini basi sitaki kamwe kujaribu kumvuta mtu kutoka katika kanisa lao. Kaa tu mumo humo kanisani mwako na ueneze Nuru. Unaona? Uwe Mkristo halisi. Mchungaji wako atakuthamini. Mtakatifu halisi, mwaminifu, na wa kweli, mtu ye yote anayemwamini Mungu atamthamini mtu kama huyo. Naam.

²⁶ Sasa, ninamshukuru ndugu huyu hapa, na mkewe, na tawi hili, kwa ajili ya nafasi hii. Na naomba tawi hili likue. Baraka za Mungu na zikae juu yake, na liwe chombo katika mikono ya Mungu, lipate kuwaokoa mamia na mamia ya watu kabla ya Kuja kwa Bwana; na ninyi matawi haya mengine yote ama wawakilishi hapa kutoka kwenye hayo matawi.

²⁷ Katika Kitabu cha Zaburi, sasa, ninataka kuzungumza juu ya somo la ajabu sa—sana, usiku wa leo, kwa muda kidogo tu. Nina Maandiko machache yaliyoandikwa hapa. Na—na nilifikiri labda kwamba, usiku wa leo, nilikuwa nikitaka kuzungumzia jambo tofauti. Lakini, naona wakati unaenda, mbona, sikutaka kuchelewa kiasi hicho, kwa hiyo nilifungua tu hapa nikapata Maandiko mengine machache. Nami ninataka kuzungumza juu ya somo la: *Unyakuo*. Unaona?

²⁸ Sasa, tunaamini ya kwamba kutakuwako na Unyakuo. Wakristo wote wanaamini jambo hilo, hiyo ni kusema wasomaji wa Biblia, wanaamini ya kwamba kutakuwako na kunyakuliwa.

²⁹ Na sasa, kusoma kwa ajili ya kuweka msingi, tutasoma Zaburi ya 25. Ninamaanisha . . . samahani. Zaburi ya 27, kifungu cha 1 hadi cha 5.

Bwana ni nuru yangu na wokovu wangu, nimwogope nani? Bwana ni ngome ya uzima wangu, nimhofu nani?

Watenda mabaya waliponikaribia, wanile nyama yangu, watesi wangu na adui zangu, wanajikwaa wakaanguka.

Jeshi lijapojipanga kupigana nami, moyo wangu hautaogopa. Vita vijaponitokea, hata hapo nitatumaini.

Neno moja nimelitaka kwa Bwana, nalo ndilo nitakalolitafuta; kwamba nikae nyumbani mwa Bwana siku zote za maisha yangu, niutazame uzuri wa Bwana, na kutaka hekaluni mwake.

Mradi atanisitiri bandani mwake siku ya mabaya, atanisitiri katika sitara ya hema yake; na kuniinua . . . juu ya mwamba.

Bwana na aongeze baraka Zake katika kusoma huko kwa Neno Lake.

³⁰ Sasa, leo, tukizungumza juu ya somo hili, na sasa huenda baadhi yenu mkatofautiana, na nji—njiia ninazoziendea. Lakini ni wangapi hapa ndani wanaoamini ya kwamba Biblia inafundisha kutakuwako na Kunyakuliwa kwa Kanisa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Naam, bwana. Hiyo ni kweli, kabisa, kuhamishwa kwa Kanisa. Kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, ama cho chote ulicho, Mpentekoste, kutakuwako na kuhamishwa.

³¹ Nami ninafikiri, katika kuzungumza, mimi—mimi sijaribu tu kusimama hapa kusema jambo fulani ambalo ninafikiria litawafurahisha watu. Sijawa na hatia ya jambo hilo. Ninataka kusimama hapa na kusema jambo fulani ninavyoongozwa kulisema, ninalofikiri litakuwa msaada kwenu, jambo fulani ambalo lingeendeleza uhusiano wenu na Mungu, kama wewe ni Mkristo; na kama wewe si Mkristo, likufanye ujionee aibu sana hata utakuwa Mkristo. Na hilo ndilo kusudi ambalo daima nimejaribu kupanga mawazo yangu, kama vile ambavyo Bwana angeniongoza.

³² Sasa, tumeonywa, kwamba Fundisho la jambo hili katika siku za mwisho litadhihakiwa. Mkiweza, hebu na tusome tu jambo hilo, kwa dakika moja tu. Liko katika II Petro, mlango wa 3. Hebu na tusome jambo hili muda kidogo tu. Mlango wa 3, na kifungu cha 3 na cha 4. Hebu na tuone hili kama sio kweli.

Mkijua kwanza neno hili ya kwamba katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wenye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe,

Na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake?... tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa.

Maana hufumba macho yao wasione neno hili, ya kuwa, zilikuwako mbingu tangu zamani, na nchi pia, imefanyizwa kutoka katika maji, na ndani ya ma... na ndani ya maji, kwa neno la Mungu.

Kwa hiyo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia.

³³ Sasa tunaona ya kwamba, sababu ya suala hili kunurishwa sana, ni kwa sababu nabii hapa amesema ya kwamba katika siku hizi za mwisho hawa wenye kudhihaki wangekuja wakisema mambo haya. Unaona? Imebashiriwa, sababu ya watu kufanya yale wanayofanya leo. Mbona, bila shaka mtu unatarajia jambo hilo, kwa sababu Biblia ilisema hivyo. “Katika siku za mwisho watakuwa wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu; wasiotaka kufanya suluhu, wasingizaji, wasiojizua, wasiopenda mema; wenye mfano wa utauwa na wakikana nguvu zake: hao nao ujiepushe nao.” Je! tunaweza kutazamia uigaji wa Ukweli? Bila shaka.

³⁴ Wakati Musa aliposhuka kwenda Misri, kuwakomboa wana wa israeli, akiwa na fimbo tu mkononi mwake kwa ajili ya uthibitisho, akiwa na Mungu wa Mbinguni nyuma yake, alifanya muujiza. Kulitokea waigaji nyuma yake, wakifanya jambo lile lile alilofanya. Unaona? Sasa, wao walifuata, baada ya yeye kufanya muujiza huo kwanza. Ndipo wakakaribia, kwa maana walikuwa wakiiga yale aliyofanya, wakiiga kitu cha kwanza. Tunaona jambo hilo.

Na sasa unasema, “Vema, hiyo ilikuwa ni katika siku za Musa.”

Lakini Maandiko yayo hayo yanasema ya kwamba watakuja tena katika siku za mwisho. “Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, vivyo hivyo watu hawa waliohairibikiwa na akili zao kuhusu ile Kweli.” Unaona? Uigaji, kila namna ya mambo ili kuwavuruga watu. Na halafu basi kama...

³⁵ Kunyakuliwa huku ambako kutatukia, na kitu cho chote ambacho Mungu alichio nacho katika njia ya Neno Lake, daima kuna kitu fulani kinachokuja kukivuruga Hicho kama wanaweza. Ni—ni—ni kusudi la Shetani kufanya jambo hilo.

³⁶ Kama vile ndugu hapa, kutoka kwenye ule mkutano huko Las Vegas, alivyosema, “Shetani alisema ulimwengu ulikuwa ni milki yake, na—na hayo yakiwa ndiyo makao yake makuu huko juu.”

Ninajua ya kwamba Shetani ndiye Mungu wa ulimwengu huu. Kila taifa chini ya mbingu linatawaliwa naye. Hiyo ni kweli

kabisa. Dunia hii ni mali ya Shetani, lakini Yesu ataichukua. Yeye aliiotoa Kwake siku moja. Naye akaikataa; lakini, Yeye alisema, maana alijua angeirithi katika wakati ujao.

³⁷ “Wenye kudhihaki.” Hebu na tuchukue kwa muda mfupi neno hilo moja, kabla hatujaenda mbele zaidi. Wenye kudhihaki!

Nilikuwa nikisoma gazeti fulani, yapata majuma mawili yaliyopita, huko Tucson, ambapo mwanamume fulani Mwingereza kutoka Uingereza alikuwa ametoa tamshi fulani. Liko kwenye kichwa cha gazeti, ya kwamba kule kusulibishwa kwa Bwana wetu Yesu Kristo kulikuwa ni njama tu, kati ya Pilato na Yesu, ya kwamba Yeye alikuja kujifanya... kujifanya tu kitu Fulani. Wala hakuna namna ambapo tungaliweza kuwakanushia hilo, kwa kuwa mambo yote ya Mungu yanapaswa kupokewa kwa imani. Hatuna budi kuamini jambo hilo. Sasa, yeye aliendelea kutoa maelezo jinsi jambo hilo lingeweza kutendeka.

³⁸ Hapa si muda mrefu uliopita, katika taifa hilo kuu, London, huko Uingereza, hasa, ambako kwamba John Wesley na Charles, na wengi wa hao wahubiri mashuhuri wa siku za mwanzoni, Spurgeon na hao wengine, walikuwa wamehubiri Injili kwenye masoko ya majani ya ng’ombe yaliyokaushwa na kila mahali kule. Waliukataa ujumbe huo wa siku zao, na basi angalia jinsi walivyo siku hizi.

Huko Ndiko ndugu Williams na hao wengine waliko usiku wa leo. Ni moja ya nchi zenye maadili machafu sana ulimwenguni. Nimesafiri kila mahali ulimwenguni, bali sijui kitu cho chote cha harau kama—kama—kama Uingereza. Ni... Billy Graham alisema jambo lile lile. Mbona, ilimbidi kumwondoa mkewe kutoka kwenye zile bustani, jinsi ma—ma—matendo ya kati ya wanaume na wanawake yalivyokuwa yakiendelea, hadharani, katika hizo bustani. Nilipokuwa kule, sijawahi kuona jambo lo lote lingeweza kuuvunja moyo wa mtu zaidi ya mambo yaliyokuwa yakiendelea huko Uingereza; ambayo ilikuwa na nafasi, na, wakati mmoja, iliongoza ulimwengu katika yale matengenezo. Inaonyesha tu jinsi inavyoweza kuanguka.

³⁹ Lakini, unaona, kile kinachosababisha jambo hilo, ujumbe uliotangazwa wakati huo, Waingereza wanajaribu kushikilia ujumbe ule kwa leo. Huo hautafaa kitu leo. Hautafaa kitu. Ingewezekanaje...

⁴⁰ Vipi kama Musa angalikuja na kuleta Ujumbe wa Nuhu, “Tutajenga safina na kuifanya iele katika Nile”? Haungefaa kitu. Na wala Ujumbe wa Yesu haungefaa kwa Musa. Na wala Ujumbe wa Wesley hautafaa wakati wa Luther; au Wes... ujumbe wa Luther, na vinginevyo.

Na leo, sisi, matengenezo yetu makuu ya mwisho yalikuwa ni Pentekoste. Na leo tunatoka kwenye hayo, wala ujumbe wa Kipentekoste hautachanganyikana na Huu, kwa maana ni siku nyingine. Lote ni Neno la Mungu, bali linajengwa. Kama vile miguu, mikono, ikija juu, inaumba Bibli-arusi kwa ajili ya Kunyakuliwa. Unaona? Hali—haliwatoi hao watu kule nyuma; waliishi katika Ujumbe wao. Wote watatoka, ambao walikuwa katika Bibi-arusi.

Kama tu vile uhai ukipitia katika ubua wa ngano. Lile ganda, lakini ngano inajiumba yenyewe kama punje ya ngano iliyoanguka ardhini.

⁴¹ Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikisoma kitabu ambacho Mjerumani fulani aliandika, na ukosoaji. Alisema, “Miongoni mwa nanii wote—mwa washupavu wote wa dini ulimwenguni, William Branham anawazidi wote.” Akasema, “Mbona, yeye si kitu ila... Yeye ni m—mchawi. Anafanya mambo haya.” Unaona, mtu huyo, akiwa hana habari.

⁴² Na, halafu basi, mtu huyo alikuwa mkosoaji. Hata hakumwamini Mungu. Alisema, “Mungu ambaye angeketi katika zile nyakati za giza, akunje mikono yake juu ya tumbo Lake, na kulicheka kundi la Wakristo; wakiwa ni akina mama, na wanafunzi Wake Mwenyewe, walivyodhaniwa; mama wakiwa na watoto wadogo na kadhalika, na kuwaacha simba wawale; na wala asiinue hata mkono.” Unaona mahali ambapo akili za kimwili, ambapo elimu na kadhalika, haviwezi kushika lile ono? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

⁴³ Hiyo punje ya ngano ilibidi ianguke ardhini. Kama tu vile ilivyombidi Yesu kuanguka, apate kufufuka tena, vivyo hivyo ilibidi kanisa la Pentekoste lianguke. Ilibidi lianguke ardhini, hizo nyakati za Giza. Ngano yo yote ambayo... punje yo yote inayoingia ardhini, haina budi kukaa katika wakati huo wa giza, ipate kuzaa.

Lakini ilianza kuchipua katika Martin Luther. Ikapitia kwa Wesley. Ikatoka ikaingia katika Pentekoste. Sasa inaingia, inatoka inaingia katika punje. Na sasa mifumo ya kimadhehebu waliyoacha nyuma, hiyo ni mabua, hivyo tu. Hauna budi kuteketezwa kwa moto, huo mfumo wa kimadhehebu. Lakini punje halisi ya ngano iliyotoka katika kila moja ya hayo matengenezo itatwaliwa katika Bibi-arusi. Yote kwa jumla itamfanyiza yule Bibi-arusi.

⁴⁴ Sasa tunaona, katika Uingereza kule, waliigiza kule kusulibishwa, si muda mrefu uliopita, kundi la watu hao, hizo ninii ndefu... vijana wadogo wenye hizo nywele ndefu na kadhalika, wakipiga mayowe, wakimwita Yesu “dadi-hoyee” na upuuzi huo wote. Ni uchafu jinsi gani!

⁴⁵ Sasa, unasema, “Huko ni London, Uingereza.”

Angalia kilichokuwa gazetini juma lililopita, hapa Marekani. Daktari fulani mashuhuri wa teolojia, kutoka katika shule nzuri, alisema ya kwamba kule ku—kusulibiwa kulikuwa ni kwa bandia. Alisema ya kwamba, “Yesu alijaribu tu kujifanya namna hiyo; ya kwamba alikuwa amekunywa mmea huu aina ya tunguja.”

Na tunaona hilo katika Mwanzo, ambapo limetajwa. Ni mmea kama bangi ama kitu kama hicho. Unapatikana katika nchi za huko Mashariki. Na kama ukiunywa, utakufanya ulale. Labda... Na uko kama mtu aliyekufa, unaanguka ghafla, kila kitu, kwa muda wa siku mbili au tatu mfululizo.

⁴⁶ Alisema, “Wakati walipompa Yeye siki na nyongo, inawezekana kabisa kwamba hayo yalikuwa ni majani ya tunguja. Nao walipofanya hivyo, walipompa hayo, basi alizimia kana kwamba alikuwa amekufa. Wakamweka kaburini, nao wakamlaza mle. Na baada ya siku mbili ama tatu, bila shaka, waliporudi, basi Yeye alikuwa ameamka tena, alikuwa amejirudia.” Kasema “Alienda huko India akafa mahali fulani, kifo cha kawaida, akijaribu kuiga dini.”

Kwanza, mkosoaji huyo, hivi watu wana nini? Unaona, ni siku hii tu tunayoishi, wenye kudhihaki, unaona, siku ya kutimiza unabii.

⁴⁷ Mungu aligawa Neno Lake kwa kila wakati, na kila mmoja wa nyakati hizo unapaswa kudhihirisha jambo hilo. Na pia aliwachagua watu tangu zamani kwa ajili ya wakati huo, kutimiza Neno hilo. Kila alipolipangia Neno Lake, Yeye alimchagua mtu fulani kwa ajili ya hilo. Alipoupangia wakati wa Musa, alimchagua Musa kwa ajili Yake. Alipopanga kipindi fulani cha kuzaliwa kwa Mwana wa Mungu, alimchagua Yeye kwa ajili Yake. Kila wakati, Yeye alimchagua mtu Wake, aliyechaguliwa tangu zamani, kama Biblia ilivyosema. Hakuna...

⁴⁸ Kama Mungu hana kikomo, Mwenyezi, mwenye nguvu zote, aliyepo kila mahali, anayejua yote, mbona, Yeye alijua mambo yote tangu mwanzo. Kwa hiyo, alijua. Hakuna kitu kilichotoka mahali pake. Sisi tu ndio tunaofikiri mambo yako hivyo. Kila kitu kinaenda. Rejea huko nyuma katika Neno Lake na tuone yale anayofanya, ndipo tutakuwa na ufahamu.

⁴⁹ Sasa, hebu wazia tu. Jambo la kwanza, kama mhudumu huyo angetumia akili, wakati walipoweka siki hiyo na nyongo mdomoni Mwake, Yeye aliitema. Kwanza, Yeye hakuinywa. Unaona? Ni wenye kudhihaki tu wanaoinuka! Jambo lingine, je! imekuwaje huyu Yesu wa Nazareti, maisha Yake yalilinganaje na kila unabii wa Agano la Kale? Ingewezekanaje? Haingaliwezekana bila ya kuchaguliwa na Mungu. Maisha Yake yalilingana na kila unabii wa Agano la Kale. Jambo lingine, kama hao wanafunzi walikuwa wamemwiga tu namna

hiyo, kwa nini kila mmoja wao alifia imani? Na hata mtume Petro alisema, “Nigeuzeni kichwa changu juu chini. Mimi sistahili kufa kama Yeye.” Jinsi walivyomchukua Andrea na kumkingamisha kwenye msalaba. Hao, kila mmoja wao, alitia muhuri ushuhuda wake kwa damu yao wenyewe. Walimwamini na kumpenda, na kutoa maisha yao kwa ajili Yake. Kama Yeye alikuwa ni mwongo, wangelipataje kufanya hivyo? Unaona? Matumizi ya kiroho, watu hawayapati.

⁵⁰ Hapa alikuwako mtu mashuhuri, si muda mrefu uliopita, Rabi fulani mashuhuri aliyeandika ya kwamba, “Musa, alipokuwa akipitia kwenye Bahari ya Shamu,” kasema, “kwa kweli haikuwa ni maji. Maji kamwe hayakufanya ukuta.” Kasema, “Jambo ni kwamba, huko mwishoni mwa Bahari ya Chumvi, kulikuwa na lundo la manyasi yaliyoshikamana. Naye akapitia kwenye hayo maji ya manyasi, manyasi ya majini. Hamna maji humo. Manyasi tu yaliyosongana, walipitia katika bahari ya—ya manyasi.” Na makasisi wengi wanaamini jambo hilo, wao, na wanalikubali.

⁵¹ Hapa si muda mrefu uliopita, wakati huyu mwanaanga wa kwanza aliporuka juu, alirudi, wala hakuwa amemwona Mungu kamwe. Hata hilo liligeuza msimamo wa wahudumu. Walidhani Mungu aliishi huko juu mahali fulani, maili mia moja na hamsini kwenda juu.

⁵² Mbona, jamani, jinsi elimu na hekima ya ulimwengu huu imegeuza kanisa likawa makusanyiko ya matambara ya nguo za manyasi! Ninii... Ni elimu na mfumo wa elimu, sayansi na ustaarabu, ni vya Ibilisi. Ni ustaarabu wa ibilisi. Biblia ilisema hivyo.

Na ustaarabu wetu ujao hautakuwa na uhusiano wo wote na ustaarabu huu, hata kidogo. Hauna uhusiano wo wote nao, hata kidogo. Utakuwa ni Ustaarabu wa tofauti, katika ustaarabu huu na ulimwengu huu wa kisayansi tulio nao. Sayansi zaidi, kadiri tunavyokuwa wa kisayansi, ndivyo tunavyoingia zaidi katika mambo ya mauti, mitego ya kuua, na kila kitu. Katika Ustaarabu ule mpya, hakutakuwako na mauti, hakuna magonjwa, huzuni, wala hakuna maumivu. Unaona? Hakutakuwa na cho chote cha huo Kule. Kwa hiyo ustaarabu huu itabidi uangamizwe, kwa maana ni wa ibilisi.

⁵³ Tunaona ya kwamba, katika Mwanzo 4, ya kwamba watu wa Kaini walianzisha ustaarabu, kujenga miji na majiji, na kadhalika, na zana za muziki, nao wakawa wanasayansi. Ndipo hao watu wakazidi kwenda mbali na Mungu, hata hivyo wakiwa ni wa kidini. Lakini wakati watu wa Sethi walipotokea, walianza kuja, kuliitia Jina la Bwana.

Aha, nena kuhusu mwenye hila!

⁵⁴ Mimi siko hapa kumuudhi mtu ye yote, kusema neno lo lote juu ya kanisa. Na kama wewe uko hapa, na ni mshirika wa

kanisa hili, sisemi jambo hili kukuudhi; maana kuna watu wengi wazuri kule, kama kulivyo nao katika makanisa mengine. Lakini nilikuwa nikisoma huko Shreveport juma lililopita, ambapo kanisa Katoliki lilitoa tamshi.

Na tunaona mahali ambapo wote wanaungana sasa kwenye baraza kuu la ekumeni, na kadhalika, kutimiza kabisa kile Biblia ilichosema watafanya. Vile vile kabisa.

⁵⁵ Sasa tunaona ya kwamba wao walisema, “Mbona, Biblia...” Baadhi ya Waprotestanti wanataka kushikilia Biblia hiyo. “Mbona,” kasema, “Biblia si kitu bali ni kitabu, ni historia ya kanisa, nao hawakuwa nayo katika jinsi ya kitabu mpaka kama miaka mia mbili na hamsini iliyopita. Kanisa limekuwepo siku zote.” Kasema, “Ilikuwa ni kanisa, wala si Biblia, na Biblia ni historia tu ya yale kanisa liliyofanya.” Ni uongo wa kijanja jinsi gani huo! Mbona, tumekuwa na Biblia kwa miaka elfu tatu. Agano la Kale liliandikwa katika Maandiko, kwa mamia na mamia ya miaka kabla ya kule kuja kwa Kristo. Ni jambo la kijanja tu la ibilisi!

⁵⁶ Nasi tunaona katika siku hii, wakati kudhihaki huku kubaya sana na kuidhihaki Biblia, na kukazana kuiondosha, Mungu hana budi kulihukumu kanisa kwa kitu fulani. Yeye hawezi kuwa mwenye haki...

Hawawezi kushuka kwenda kwenye barabara hii na kunikamata, na kusema ninaendesha maili thelathini kwa saa katika eneo la maili ishirini, isipokuwa pawe na kitu fulani pale cha kuniambia ya kwamba nimeruhusiwa tu kuendesha maili ishirini. Hakina budi kuwapo.

Na Mungu atalihukumu kanisa, atawahukumu watu, siku moja. Tunajua jambo hilo. Kuna hukumu inayokuja. Kwa hiyo kama atalihukumu kwa kanisa Katoliki, ni kanisa Katoliki lipi? Kama atalihukumu kwa Methodisti, la Kibaptisti limepotea. Akilihukumu kwa la umoja, la uwili limepotea. Unaona? Atalihukumu kwa kitu gani? Alisema atalihukumu kwa Kristo, na Kristo ni Neno. Kwa hiyo Neno la Mungu, ndilo Mungu atakalohukumia. “Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu. Yeye yule jana, leo, na hata milele.” Unaona? Kwa hiyo, atalihukumu kwa Neno Lake.

⁵⁷ Na sasa tunaona ya kwamba katika siku hii, wakati wanapojaribu kusukumia Biblia nje, “Likubali kanisa. Biblia; hatuitaki. Kanisa,” kwa hiyo wanaweza kufanya namna yo yote ya kanuni ya imani ama cho chote kile, na kutembea kwayo.

⁵⁸ Vema, kama nilivyokuwa nikizungumza hivi majuzi usiku huko Shreveport. Katika zile—ule ushirika wakati walipomwua yule mwana-kondoo wa sadaka, hakukupaswa kuwe na “chachu miongoni mwao, katika sikuzote hizo saba,” hakuna chachu, hakuna mkate uliotiwa chachu. Kila kitu kilipaswa kisiwe

na chachu. Hiyo iliwakilisha zile Nyakati Saba za Kanisa tunazopata kwenye kitabu hapa, wala hakuna chachu. Ati nini? Ni kitu fulani kuchanganywa Nalo. Nasi tunachanganya kanuni za imani na madhehebu, na mambo mengine yote, pamoja na Neno, na bado tunajaribu kuliita kwamba ni Neno. “Hakutakuwko na chachu katika siku zote hizo saba.”

⁵⁹ Na hata kile kinacholiwa leo, usijaribu kukiweka mpaka kesho. “Kiteketezeni kwa moto, kabla hakujapambazuka,” kwa maana kuna ujumbe mpya unaokuja, na jambo jipya. Unaona, kujaribu kukihifadhi, lakini huo umekuwa ndio msimamo wa kanisa. Ufufuo unatokea, na muda si muda, mnamo miaka kama mitatu hivi, wanaanzishia shirika juu yake. Madhehebu yanazuka, shirika fulani.

Lakini umeona? Huu umekuwa ukisambaa kwa miaka ishirini sasa, wala hakuna shirika lo lote. Wala halitakuwako. Huu ni mwisho. Ngano imeirudia ngano tena. Ngano imeirudia punje yake tena. Ganda limeachana nayo. Nayo ngano haina budi kukaa kwenye uwepo wa jua, ipate kuivishwa.

⁶⁰ Je! si ni jambo la ajabu, ya kwamba, si muda mrefu uliopita huko kwenye Pwani ya Mashariki, lile giza lililofunika kote kote? Hawakuweza kufahamu jambo hilo. Umeme ulikatika kote huko Texas, wiki jana. Hawawezi kufahamu jambo hilo. Je! hamtambui ya kwamba hiyo ni ishara? Hivi hamjui ya kwamba mataifa yanavunjika? Israeli iko katika nchi ya uenyeji wake. Na ishara hizi zinaonyesha ya kwamba tuko katika wakati wa mwisho. Wakati huo huo umeme unakatika, je! hamjui hiyo ni ishara ambayo nabii alisema? Naam. “Lakini itakuwa Nuru mnamo wakati wa jioni,” ya kwamba kutakuwako na Nuru fulani itakayotokea katika wakati wa jioni, wakati giza tupu na kadhalika litatokea jinsi linavyotokea sasa.

⁶¹ Angalia tu jinsi umeme ulivyokatika. Papa ndio kwanza aje hapa.

Kumbukeni, kule maskanini, wakati hao...ninyi mna kanda. Ninaamini, ninyi nyote mnazichukua. Jinsi ambavyo Bwana alionesha pale siku ile, maskanini, pale hasa ambapo hizo nyakati za Kanisa zilipokuwa na jinsi ambavyo zingekuwa! Nami nilizichora kwenye ubao kule, hizo nyakati za kanisa ambazo mnazona hapa zimechorwa katika kitabu. Na kama huyo Roho Mtakatifu hakushuka katika Nguzo kubwa ya Moto, na akaenda moja kwa moja nyuma pale ukutani na kuzichora, Yeye Mwenyewe, wakati watu mia tatu au mia nne walipokuwa wameketi, wakiiangalia!

Na mara papa alipoanza kuja huku, mwezi kwa namna fulani ukawa giza tupu. Nao wakapiga picha zao jinsi ile ile zilivyochorwa pale jukwaani. Sasa yeye amefanya ziara yake hapa tarehe kumi na tatu, akapiga hatua kumi na tatu, akawapa ushirika watu kumi na watatu, kwa taifa ambalo ni namba kumi

na tatu, na giza tupu likiingia kila mahali. Je! hamwoni mahali tulipo? Tuko katika wakati wa mwisho.

⁶² “Wenye kudhihaki watainuka katika siku za mwisho, wakisema, ‘Hakuna tofauti katika wakati huu na wakati uliopita, na wakati baba zetu walipolala mauti.’”

Lakini mtakapoonza mambo haya yakianza kutukia, inueni kichwa chenu; iweni tayari. Jambo fulani linaweza kutokea wakati wote. Kristo akija kuchukua Kanisa Lake.

⁶³ Sasa, hao hawaamini hayo, kwa maana ni...hiyo ni... Wao, wao wanapas-...Hawatambui ya kwamba wao ndio wanaoyatimiza Maandiko. Watu kwa kweli hawatambui jambo hilo, wakifanya mambo haya na kusema mambo haya, wanatimiza Maandiko.

Jinsi kuhani mkuu Kayafa, na makuhani hao wote katika siku hiyo, waliomdhihaki na kumfanyia mzaha, hawakujua ya kwamba, Mungu yeye yule ambaye walikuwa wakiimba habari Zake, “Mungu Wangu, mbona umeniacha?” Zaburi 22, “Mikono Yangu na miguu yangu waliitoboa.” Wakiimba hayo hekaluni, na huku Yeye anakufa pale nje msalabani. Hawakujua hata kidogo walikuwa wanafanya jambo hilo. Hata Yesu aliomba, “Baba, wasamehe. Hawajui watendalo.” Kwa sababu, kwa kweli walikuwa wamebashiriwa, na Maandiko, kuwa vipofu.

⁶⁴ Hivi mlijuu kanisa la Kiprotestanti na la Katoliki limebashiriwa, katika siku za mwisho, kuwa kipofu, jambo lile lile, katika Maandiko, huku Kristo akiwa nje, akijaribu kuingia ndani? “Kwa sababu unasema, ‘Mimi ni tajiri, wala sina haja ya kitu,’ hujui ya kuwa wewe u mnyonge, maskini, mwenye mashaka, uchi, na kipofu, wala hujui,” Ufunuo 3. Haya basi, wamerudi kwenye upofu tena, wakikanyaga vitu vya Mungu, kana kwamba (wao) hivyo havikumaanisha kitu kwao, kuvidhihaki na kuvifanyia mzaha. Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

⁶⁵ Lakini, kwa Kanisa, Bibi-arusi, Kunyakuliwa ni ufunuo kwake. Kumefunuliwa kwake. Kwamba, huo ufunuo, Bibi-arusi wa kweli wa Kristo atakuwa akingojewa ufunuo huo wa Kunyakuliwa.

⁶⁶ Sasa, ni ufunuo, kwa maana ufunuo ni imani. Huwezi kuwa na ufunuo bila huo kuwa imani. Imani ni ufunuo, kwa maana ni jambo fulani lililofunuliwa kwako. Imani ni ufunuo. Imani ni kitu fulani ambacho kimefunuliwa, kama ilivyokuwa kwa Ibrahimu, ambaye aliweza kuita kitu cho chote kilichokuwa kinyume cha yale aliyokuwa amefunuliwa, kana kwamba hakikuwa hivyo. Sasa, imani, hivyo ndivyo imani ilivyo, ni ufunuo wa Mungu. Kanisa limejengwa juu ya ufunuo, mwili wote mzima.

⁶⁷ Hapa majuma machache yaliyopita, nilikuwa nikizungumza na mhudumu Mbaptisti mzuri. Alikuwa kujadiliana nami.

Alisema, “Ninakupenda kama mwanadamu, lakini,” kasema, “wewe umechanganyikiwa kabisa.”

Nikasema, “Basi, ninaomba unisaidie kuniweka sawa.” (akasema . . .) “kwa Maandiko.”

Akasema, “hatutaweza kamwe, Ndugu Branham, kukubaliana katika mambo haya mpaka tutakapoweka kila neno juu ya neno juu ya neno likubaliane na Kiyunani, na kadhalika.”

⁶⁸ Nikasema, “Loo, bwana, unajua vema zaidi kuliko hilo.” Nikasema, “Hata katika lile Baraza la Nikea, huko nyuma kabisa umbali huo, miaka mia tatu tangu kifo cha Kristo, wao walikuwa wangali wanahojiana kwamba ni mwanachuoni gani wa Kiyunani alikuwa sahihi. Huwezi kujua. Ni ufunuo, jambo hilo lote. Ni ufu- . . .”

Akasema, “Mimi siwezi kukubali ufunuo.”

Nikasema, “Basi unawezaje kumkubali Kristo?”

Akasema, “Mbona, Biblia ilisema, ‘Yeye amwaminiye ni . . . Yesu Kristo, yuna Uzima wa Milele.’”

⁶⁹ Nikasema, “Hiyo ni kweli. Inasema pia ya kwamba hakuna mtu anayeweza kukiri Yesu ni Kristo ila tu kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu ambao mtu huyo amefunuliwa.” Unaona? Haya basi, linarudi nyuma tena moja kwa moja, linarudi moja kwa moja kwenye ufunuo. Linapaswa kufunuliwa, katika Biblia.

⁷⁰ Kaini na Habili hawakuwa na Biblia ya kusoma, lakini ilifunuliwa kwa Habili, kwa imani, ambayo ni ufunuo. Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi kuliko ile ya Kaini. Ambapo, Mungu alishuhudia kwamba alikuwa mwenye haki.

Yesu alipoulizwa hapa, Mathayo 16:17 na 18. Hatuna wakati wa kulisoma, lakini kama ukitaka kuliandika. Yeye alisema, “Watu husema kwamba Mimi, Mwana wa Adamu, ni Nani?”

“Mmoja wao alisema, ‘Wewe ni Musa, Eliya, ama kadhalika.’”

Yeye akasema, “Lakini ninyi mnasema kwamba Mimi ni Nani?”

⁷¹ Akasema, “Wewe ndiwe Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.”

⁷² Akasema, “Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Juu ya mwamba huu,” ufunuo wa kiroho wa Mungu ni Nani, kwamba Yesu ni Nani. Naye ni ufunuo wa Mungu, Mungu aliyefanyika mwili na kufunuliwa kwa ulimwengu.

“Yeye alikuwa katika ulimwengu. Mungu alikuwa katika Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake, akifunua jinsi Mungu alivyokuwa, katika mwili wa nyama.”

“Wewe ndiwe Kristo, Mtiwa Mafuta, Mwana wa Mungu.”

⁷³ Yeye akasema, “Mwili na damu havikukufunulia hili kamwe, bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia hili. Juu ya mwamba huu, nitalijenga Kanisa Langu, ufunuo wa Neno katika majira Yake. Nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda.”

⁷⁴ Kitabu cha Ufunuo ndicho Kitabu cha mwisho cha Biblia. Kimetiwa muhuri kwa wasioamini. Humo ndani, Biblia inasema, katika mlango wa 22, “Ye yote atakayeondoa neno moja kutoka Kwake, ama kuongeza neno moja Kwake, Mimi nitamwondolea sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima.” Tunatambua ya kwamba, basi, Hicho kwa jumla kilitolewa kwa waaminio. Na kinafungua Kitabu cha Ufunuo na kufunua kwamba Mwandishi wa Kitabu hiki kizima ni Nani. “Yeye anaonekana kama Alfa na Omega,” tangu mwanzo hadi Ufunuo, Yesu Kristo yeye yule, moja kwa moja katika kitabu kizima. Naye anafunua siri nzima ya utu Wake na mipango Yake kwa ajili ya nyakati Zake za kanisa ambazo zinakuja, nayo ilifungwa mle ndani kwa Mihuri Saba.

⁷⁵ Sasa, Kitabu hiki kiliandikwa, lakini basi, kumbuka, kilitiwa muhuri kwa Mihuri Saba. Na Mihuri hii Saba haikuwa ifunguliwe, (Ufunuo 10) hadi kule kutangaza kwa yule malaika wa mwisho mwanadamu hapa duniani, Ufunuo 10:7. Unaona? “Na katika siku za kutangazwa kwa Ujumbe wa malaika wa mwisho, malaika wa saba, siri ya Mungu itatimia katika wakati huo.” Hiyo, na huo ndio wakati tunaishi.

⁷⁶ Sote tunajua tunaishi katika wakati wa Laodikia. Kamwe hakutakuwa na wakati mwingine zaidi. Haiwezekani. Kwa hiyo, tunaishi katika wakati wa Laodikia. Na hii Mihuri Saba ambayo imeshikilia Kitabu hicho, ni siri kwa watu, kinapaswa kufunguliwa katika siku hiyo. Hivyo ndivyo alivyoahidi. Sasa, haitakuwa ni jambo lo lote nje ya Neno, kwa kuwa huwezi kuongeza kwenye Neno wala kutoa kutoka kwenye Neno. Halina budi kudumu Neno daima. Lakini ule ufunuo utafunua Kweli Yake, kwamba ni nini, kuifanya ikubaliane na Maandiko hayo mengine. Ndipo Mungu anathibitisha kwamba jambo hilo ni Kweli. Unaona?

⁷⁷ Mungu hahitaji mfasiria ye yote. Yeye ndiye anayejifasiria. Yeye hujifasiria Mwenyewe kwa kutimiza mambo ambayo Yeye alisema yangetimia. Kama vile, hapo mwanzo, Yeye alisema, “Iwe nuru,” na nuru ikawa. Hilo halihitaji tafsiri yo yote. Lilithibitishwa.

⁷⁸ Sasa, Yeye aliahidi mambo fulani fulani katika siku hii ya mwisho, katika Maandiko. Mbona, ndiyo hayo hapo.

Hivyo ndivyo Yesu alivyokuwa Mwana wa Mungu. Yeye aliahidi kumtuma. Wakati alipokuwa hapa duniani katika siku Zake, nao watu hawakuweza kumwamini, Yeye alisema,

“Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, Nayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Kama sizitendi kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi. Lakini kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini kazi nizifanyazo, maana zinashuhudia kwamba Mimi ni nani.”

⁷⁹ Vema, basi, katika wakati wa Wesley, kazi alizofanya zilishuhudia kwamba yeye alikuwa ni nani.

Katika wakati wa Luther, kwenye yale matengenezo, mbona, hakika, zilishuhudia kwamba yeye alikuwa ni nani.

⁸⁰ Katika siku za Wapentekoste, kule kurudishwa kwa karama, kurudishwa kwa karama, kunena kwa lugha na kutoa pepo, na karama, mbona, ilishuhudia. Hakukuwako na utani juu ya jambo hilo. Watu walisema, wakati jambo hili lilipozuka mara ya kwanza... Nilisoma vitabu juu ya historia ya Pentekoste. Walisema, “Hauwezi kudumu muda mrefu. Utazima.” Ungali unalipuka moto. Kwa nini? Ni kwa sababu hutaweza kamwe kuuzima. Mungu alisema utakuwako. Ni ile sehemu ya Neno, wala usingeweza tena kuuzima huo.

Na tena wakati Bibi-arusi anaitwa atoke, utauzimaje? Ni ufunuo wa dhihirisho la Neno likifanywa halisi. Nasi tunaishi katika siku hiyo; Mungu asifiwe; Ufunuo wa siri ya Yeye Mwenyewe.

⁸¹ Sasa, kunyakuliwa ni ninii tu...Kunyakuliwa huku tunakonena habari zake ni kwa ajili ya Bibi-arusi peke yake. Kumbukeni, Biblia ilisema, “Na hao wafu waliosalia hawakuishi tena kwa muda wa miaka elfu.” Kunyakuliwa huku kukuu! Kama hakuna Kunyakuliwa, rafiki zangu, tuko wapi? Tutafanya nini? Tunaishi katika wakati gani? Tuna ahadi gani? Kutakuwako na Kunyakuliwa. Biblia inasema kutakuwako. Nako kutakuwa tu ni kwa wateule, Bibi Mteule, Bibi-arusi wa siku hii ambaye ametoka, lile Kanisa.

⁸² Neno lenyewe *kanisa*, linamaanisha “walioitwa watoke.” Na kama vile ambavyo Musa aliita taifa kutoka katika taifa, Roho Mtakatifu anaita Bibi-arusi kutoka katika kanisa; Kanisa kutoka katika kanisa; washiriki, kutoka katika kila madhehebu wakifanyiza Bibi-arusi, Mti wa Bibi-arusi. Uko kwenye—kwenye kanda, ule *Mti wa Bibi-arusi*. Bibi-arusi ameitwa atoke, anaitwa, na huyo ndiye ambaye ndiye huo Mti wa Bibi-arusi. Bibi-arusi, hasa, ndiye atakayekuwa katika Unyakuo; huyo, peke yake, hakuna mwingine ila Bibi-arusi, mteule aliyekwisha julikana na Mungu tangu mwanzo, jeni ya kiroho ya Baba.

Hebu nisimame hapa kwa dakika moja. Na ninazidi kuwa na wasiwasi, nikifikiri nitawachelewesha, nitawachelewesha kupita kiasi.

⁸³ Lakini, angalia, tazameni, kila mmoja wenu ninyi watu. Je! unajua, miaka kadha kabla hujazaliwa, ulikuwa ndani ya baba yako kama jeni? [Kusainyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo ni

kweli. Seli zazi, mbegu, ilikuwa ndani ya baba yako; inatokana na jinsia ya mwanamume, si ya mwanamke. Unaona? Mwanamke ndiye anayetoa yai, tuta. Lakini ile seli zazi inatokana na ba- . . . Sasa, tuseme katika baba yangu. . .

⁸⁴ Ama, mwanangu anayeketi hapa, nilipokuwa na umri wa miaka kumi na sita, mwanangu alikuwa ndani yangu. Sikumjua, lakini alikuwako. Sasa, kupitia kwenye tuta, kupitia ndoa takatifu, yeye anakuwa sura yangu. Ninamjua. Ninaweza kushiriki pamoja naye. Naye alitokea tu katika wakati uliokubalika.

⁸⁵ Sasa, vivyo hivyo na wewe ulikuwa ndani, kama una Uzima wa Milele, ulikuwa ninii. . . katika Mungu kabla hapajakuwako na ulimwengu. Wewe ni sehemu, mwana wa Mungu, sifa za Mungu. Yeye alijua wakati hasa uliokuwa wewe utokee. Alikuchagua tangu zamani kwa ajili ya wakati huo, upate kupachukua mahali hapo, wala hakuna mtu mwingine anayeweza kupachukua; sijali ni waigaji wangapi na kadhalika. Huna budi kuwa pale, kwa maana Yeye alijua ungekuwako. Sasa, wewe umedhihirishwa. Sasa unaweza kushiriki pamoja Naye, na hivyo ndivyo Yeye anavyotaka. Yeye anatamani sana ushirika, kuabudiwa. Lakini kama maisha yako hayakuninii. . . daima hayakuwa ni sifa ndani ya Mungu, wewe ni mwigaji tu wa Ukristo. Unaona? Kutakuwako na mabilioni na mabilioni yao, watakaokuwa tu ni waigaji wa Ukristo.

⁸⁶ Tamshi nililotoa hivi majuzi tu. Nilikuwa nikimwangalia Ndugu Demos Shakarian kule, wakati walipokuwa wakizalisha ng'ombe machotara, nikaona tyubu za majaribio, na kadhalika, zikiingizwa na madaktari, nami nikiangalia mambo haya.

⁸⁷ Katika kutoka kwa kawaida kwa mbegu za kiume, kuna kama seli zazi milioni moja zinazotoka kutoka kwa dume kila wakati. Na kadiri ya mayai milioni moja yanatokana na jike wakati—wakati huo huo. Lakini je! ulijua, katika hizo zote seli zazi ndogo zinazosogea kuzunguka hapo, milioni moja ya hizo, kuna moja tu iliyochaguliwa kupata uhai, na kuna yai moja tu lililorutubishwa? Na seli zazi hiyo ndogo itatambaa moja kwa moja kupitia katikati ya hizo seli zazi nyingine zote ndogo, moja kwa moja juu ya kila seli zazi ndogo inayofanana nayo, na kupanda juu ya hiyo na kuja hapa, na kupata hilo yai lililorutubishwa na kujipenyeza ndani yake. Ndipo hizo nyingine zote zinakufa. Mbona, nena kuhusu uzazi wa kibikira, loo, huko hata si nusu ya siri za uzazi wa kimwili, jinsi kulivyokusudiwa hapo kabla, kukachaguliwa tangu zamani na Mungu!

⁸⁸ Sasa, hapo mwanzo, kule nyuma kabisa, miaka mingi sana iliyopita kabla wakati haujaanza, wewe, kama wewe ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, usiku wa leo, ulikuwa ndani ya Mungu wakati huo, Baba yako. Hiyo ndiyo sababu, wakati ulipokuja katika maisha haya hapa na kukiri Ukristo, vema, kila kitu

kikienda kombo, hukujua ni kwa nini imekuwa *hivi*, na yote *haya*. Hiyo, hukujua jambo hilo. Lakini, siku moja, kitu Fulani kilikugusa. Kilikuwa ni nini? Uhai huo uliokuwa kule ndani, tangu mwanzo. Na kama . . .

⁸⁹ Kama hadithi yangu ndogo kuhusu yule tai, kumpata, mama yake akimpata huyo tai. Mmenisikia nikihubiri juu ya jambo hilo, jinsi maskini kifaranga huyo wa tai kilivyoanguliwa chini ya kuku. Lakini yeye, tabia zake za kujaribu kuwalisha hao— hao kuku, maskini tai huyo mdogo asingeweza kuvumilia jambo hilo, kwa maana yeye, kwanza, hakuwa kuku. Hata hivyo, alikuwa kizizini pamoja na hao kuku, na akawafuata hao kuku. Lakini yeye angekwaruza katika hilo eneo la ghala na kadhalika, na maskini kifaranga huyo wa tai asingeweza kuvumilia jambo hilo. Lakini kila wakati angefanya mlío wa kuku na kila kitu, maskini kuku wote wadogo wangeenda, kwa hiyo naye angeenda, pia. Lakini siku moja . . .

⁹⁰ Mama yake alijua ya kwamba alikuwa ametaga mayai mawili, si moja. Lazima kulikuwa na lingine, mahali fulani. Akaenda kulitafuta, akiruka kuzunguka kila mahali, akizunguka-zunguka. Hatimaye akafika kwenye eneo la ghala, ndipo akamwona mtoto wake, ndipo akampigia makelele. Ilikuwa ni sauti, ambayo, alitambua ya kwamba hicho ndicho kitu kinachoenea. Hicho ndicho anachotafuta, unaona, ndipo akatambua basi ya kwamba yeye hakuwa kuku. Alikuwa ni tai.

Na hivyo ndivyo ilivyo, kila Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, unapokuja. Sijali ni madhehebu mangapi uliyojiunga nayo, ni majina mangapi, uliandika jina lako kwenye vitabu na kadhalika. Wakati Neno hilo halisi la Mungu linapothibitishwa na kuonyeshwa ni la kweli mbele zako namna hiyo, unatambua wewe ni tai, papo hapo. Kwa sababu, huu mlío wote wa kuku, “Hebu ujiunge na *hili*, na ujiunge na *hili*, na kuenda *hivi* na *vile*,” ni upuuzi. Ni kuongeza kwa kweli Neno kwa Neno.

⁹¹ Wakati seli zazi inapoingia katika tumbo la uzazi la—la mwanamke, halichukui. . . Wewe, wewe hukufanyika seli zazi ya binadamu kutoka kwa baba yako, halafu tena kitu kinachofuata unakuwa seli zazi kutoka kwa mbwa, na halafu tena kutoka kwa paka, na halafu tena kutoka kwa kuku. Yote nzima ilikuwa ni seli zazi ya kibinadamu.

Nao Mwili wa Yesu Kristo, yule Bibi-arusi, utakuwa ni sehemu ya Mwili Wake. Ambao utakuwa . . . Yeye alikuwa ni Neno, naye Bibi-arusi itampasa kuwa Neno; Neno likiongezwa kwenye Neno, lililoongezwa kwenye Neno. Kuhesabiwa haki kwa Luther, kutakaswa kwa Wesley, ubatizo wa Kipentekoste wa Roho Mtakatifu, kurudishwa kwa karama, na hayo mengine yote, yanaambatana Nayo. Unaona? Haina budi kuwa ni Neno juu ya Neno, seli zazi juu ya seli zazi, Uhai juu ya Uhai, ili

kuleta kimo kikamilifu cha Bibi-arusi wa Bwana Yesu Kristo. Sasa unakumbuka, wewe ulikuwa ni sifa.

⁹² Na sasa, jambo ni kwamba, baada ya sisi kutambua mambo haya, ya kwamba Kristo anakuja kwa ajili ya Bibi-arusi Wake, sasa tunaingiaje katika Bibi-arusi huyo? Sasa, hilo ndilo swali.

Wengi husema, “Jiunge na kusanyiko letu.” Moja ya hayo linataka ubatizo wa aina fulani. Moja linataka kufanya *hivi* ama *vile*. Moja lilisema, “Huna budi kunena kwa lugha, la sivyo hujampata.” Hilo lingine lilisema, “Si lazima unene kwa lugha.” *Hili* linasema, “Lazima ucheze katika Roho.” Na *hili* linasema, “Yapasa kupiga makelele.” *Hili*, “Lina mhemko.” Yote ni sawa, na halafu, bado, hayo yote yamekosea.

Mtu ambaye ameninii...ama mwanamke, ama mtoto wa Mungu, aliyezaliwa na Roho wa Mungu, anawezaje kukana Neno la Mungu? Wakati, Mungu Mwenyewe alilifasiri na kusema, “Hili ndilo. Nililiahidi. Hili hapa,” akilionyesha waziwazi tu linavyoweza kuwa. Kumbe, hawana budi kuliona. Unaona? Kristo angewezaje kukana Neno Lake Mwenyewe? Na iwapo Kristo yumo ndani yako, Yeye hawezi kukana Neno Lake Mwenyewe.

⁹³ Basi tunaingiaje kwenye mwili huu? Wakorintho wa Kwanza 12, “Kwa roho mmoja sote tumebatizwa kuwa katika Mwili huu, kwa ubatizo mmoja wa Roho Mtakatifu.” Na hilo, kama unataka kuliandika, ni Wakorintho wa Kwanza 12:13. “Na kwa Roho mmoja sote tumebatizwa.” Na Roho ni Uzima wa Kristo. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Uzima wa Kristo! Na uzima wa mbegu yo yote...Ambapo, Yeye alikuwa ni Neno Mbegu, kunaihuisha hiyo Mbegu. Unalipata? Kama huo—kama huo Uhai unakaa kwenye Mbegu, na ubatizo huu wa Roho Mtakatifu unakuja juu Yake, hauna budi kuleta Uhai wa Mbegu hiyo.

⁹⁴ Kama nilivyowaambia, hapa Phoenix, si muda mrefu uliopita. Nilikuwa nikizungumza na Ndugu John Sharrit. Nami nilikuwa huko nje, naye akanionesha mti fulani, aina ya mchungwa. Yeye ali—alikuza matunda chungwa mengi sana. Naye alinionesha mti mmoja, uliokuwa na aina ya matunda chungwa nane ama tisa mbalimbali. Ndipo nikasema, “Ndugu Sharrit, huu ni mti wa aina gani?”

Kasema, “Mchungwa.”

Nikasema, “Kwa nini limau, na kangaja, na chenza na balungi?”

Yeye akasema, “Yote ni aina ya matunda chungwa; yamepandikizwa.”

“Loo,” nikasema, “Naona. Sasa, mwaka ujao, wote utazaa machungwa. Kwa sa-...”

⁹⁵ “Loo, la. Kila mti utazaa aina yake. Kila tawi litazaa tunda lake lenyewe.”

⁹⁶ Wengi wenu ninyi wakulima wa matunda mnajua jambo hilo, hapa katika bonde hili la matunda aina ya machungwa. Litazaa kwa jinsi yake lenyewe. Ukiweka tawi la mlimau kwenye mchungwa, litazaa limau, kwa maana lina asili ya jamii ya tunda chungwa. Hata hivyo, halitazaa tunda la asili.

Na hivyo ndivyo tulivyofanya. Tumepandikiza, tukachukuana na kanuni za imani, na kadhalika, na kupandikiza katika kila moja, Hapa. Wamethodisti wanawezaje kuzaa cho chote ila mtoto wa Kimethodisti? Madhehebu yo yote yanawezaje kuzaa cho chote isipokuwa mtoto wa kimadhehebu?

⁹⁷ Lakini kama mti huo ukiwahi kuzaa tawi la asili, tawi hilo litazaa machungwa.

Na halafu kama Mungu akiwahi kufanya jambo lo lote katika Kanisa, litakuwa ni kurudi kwa la asili, pamoja na Neno tena. Kweli kabisa. Lazima iwe hivyo, maana ule uhai uko katika huo mti, na unazaa ya aina yake.

⁹⁸ Sasa, tunapoona, sasa, kuna lile kanisa kubwa lililoenda, kupitia katika nyakati nyingi likizaa matunda yake. Na wakati matawi yanapokwisha, watu huyakata na kuyaondoa. Katika Yohana Mtakatifu 15 hakuupogoa ule mzabibu, sasa. Yeye aliyaondoa matawi, akayakata, kwa maana hayakuwa yakizaa matunda yo yote. Na—nasi. . .

⁹⁹ Yesu anataka matunda kwa, kwa ajili yake Mwenyewe. Mke Wake hana budi kuzaa watoto walio kama Yeye.

Basi, kama hawatawazaa watoto, watoto Bibi-arusi, watoto Neno, basi ni mtoto wa kimadhehebu. Basi, upendo wake wa kwanza, kwa ajili ya ulimwengu na madhehebu, yeye anarudi huko. Nao hawawezi kuzaa Mkristo halisi, wa kweli, aliyezaliwa mara ya pili, maana hakuna kitu pale cha kumzaa.

¹⁰⁰ Ni kama tu ukichukua tawi la mlimau na kulipandikiza humo; litazaa limau, bali haliwezi kuzaa chungwa, kwa maana halikuwapo pale tangu mwanzo. Bali mchungwa ulichaguliwa hapo mwanzo, kujua tangu zamani kwa Mungu, kuliuchagua tangu zamani na ukazaliwa, hauna budi kuzaa chungwa. Hauwezi kuzaa kitu kingine.

¹⁰¹ Hivyo ndivyo ilivyo kwa Kanisa la Mungu aliye Hai, wakati ile saa inapowadia. Kila mtu. . . Hebu Mungu aanze kufanya jambo fulani, kila mtu anachukua mpira na kukimbia nao. Unaona? Daima imekuwa hivyo.

Nilikuwa nikisoma katika historia, ya Martin Luther, hapa si muda mrefu uliopita. Ilisema, “Ninii. . . Haikuwa ni vigumu sana kuamini ya kwamba Martin Luther angeweza kupinga kanisa Katoliki na kufaulu. Bali,” ilisema, “jambo la ajabu, ni kwamba yeye aliweza kusimama imara juu ya wazimu wote

uliofuata ufufuo wake, na hata hivyo adumu mwaminifu kwenye kuhesabiwa haki kwake.” Unaona? Ni kila kitu tu, maigo na kila kitu, vilimfuata.

¹⁰² Angalia Bi. Semple McPherson, Aimee Semple McPherson, aliyekuwa na hekalu hili hapa. Kila mwanamke mhubiri alikuwa na hayo mabawa, na alishika Biblia kwa mtindo ule ule, ma—maigo tu ya kimwili!

Hawawezi kuwa wa asili. Hivyo ndivyo makanisa yasiyoweza kuwa. Hebu acha kanisa moja lipate kitu cho chote kile mjini, hilo kanisa lingine haliwezi kuvumilia jambo hilo. Wanakipata. Unaona? Wao si wa asili tena.

Neno la Mungu ni la asili. Ni Neno, Nalo halina budi kuzaa ya—ya aina Yake; aina Yake katika majira Yake, limeteuliwa, limechaguliwa tangu zamani na Mungu, Baba.

¹⁰³ Sasa, tunaingiaje katika Kanisa hili? “Kwa Roho Mmoja sote tumebatizwa kuwa Mwili huu mmoja, Mwili wa Kristo,” ambao ni Bibi-arusi, lile Neno. “Tumebatizwa mle ndani na Roho Mtakatifu.”

¹⁰⁴ Sasa hebu na tuone kama tuko katika wakati wa mwisho, ama la. Sasa tunaona, kama tukifungua nyuma katika Mwanzo, kwenye ninii, loo, kwenye mlango wa 5, mnaweza pia kufungua katika Luka muone, ya kwamba Henoko alikuwa wa saba kutoka kwa Nuhu. Henoko.

Hapo inafunulia ule uzao wa nyoka, kwa maana kama Kaini alikuwa ni mwana wa Habili, basi alikuwa ni wa nane. Unaona? Lakini hakuna mahali po pote katika Biblia ambapo imenenwa ya kwamba Kaini alikuwa ni Mwana wa Habili—ama Kaini—ama Kaini kuwa ni mwana wa Adamu. Kwa maana kwamba Biblia ilisema, “Yeye alikuwa ni wa yule mwovu.” Na Adamu hakuwa yule mwovu. Unaona? “Yeye alikuwa ni wa yule mwovu.”

¹⁰⁵ Sasa tunaona hapa ya kwamba Henoko alikuwa wa saba kutoka kwa Nuhu, ambaye alikuwa ni mfano wa zile nyakati za kanisa. Sasa, hao watu wengine wote sita, waliomtangulia, walikufa, bali Henoko alihamishwa. Henoko alinyakuliwa, huyo wa saba, ikionesha ya kwamba Wakati wa Saba wa Kanisa ndio wenye Kunyakuliwa. Sasa, hapana shaka ya kwamba tuko kwenye wakati wa saba wa kanisa. Sote tunajua jambo hilo.

¹⁰⁶ Sasa, ni Wakati wa Saba wa Kanisa ndio unaotwaliwa katika Unyakuo. Hizo zingine sita zilikufa. Bali Henoko alinyakuliwa, kwa kuwa, “Hakuonekana. Mungu alimchukua.” Bali Henoko, alinyakuliwa, alikuwa ni mfano wa hao wengine wote wakifa, bali Bi—Bibi-arusi wa wakati wa mwisho ataitwa atoke. . . Kule kunyakuliwa, bila kuona mauti, ataitwa kutoka kwenye wakati wa saba wa kanisa, ambapo sisi sasa tunashuhudia wakati huo. Loo, jamani! Hebu na tulichambue sasa, kwa kindani sana. Unaona?

¹⁰⁷ Sasa, hapa, pia, mfano wa nyakati saba za kanisa, ambapo katika Ufunuo 10:7, ile siri kuu ya kile Kitabu ilikuwa ifunguliwe na Ujumbe wa malaika wa saba.

¹⁰⁸ Sasa, kuna Mjumbe juu ya haya yote, daima, na mjumbe duniani. Neno la Kiingereza *malaika* linamaanisha “mjumbe.” Na katika Ujumbe wa malaika wa saba, alipokuwa akitoa matangazo yake, huduma yake, “basi alipoanza kutangaza huduma yake,” si wakati alipoanza kutoka nje.

Yesu wakati alipoanza kutoka nje, Yeye alianza kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka. “Loo, huyo Rabi mashuhuri! Yeye Nabii!” Na kila mtu alimtaka kanisani kwake.

Bali wakati alipoketi chini siku moja, na kusema, “Mimi na Baba Yangu ni Mmoja,” hilo lilikuwa ni jambo lingine. Hilo lilikuwa ni jambo lingine. “Na msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa Damu Yake, hamna uhai ndani yenu.”

“Kumbe, Yeye ni kizuu kifyonza damu!” Unaona? Unaona? Hilo lilikuwa ni jambo lingine.

Yeye hakulielezea. Walikuwa tayari wameona dhihirisho, thibitisho la Neno la Mungu kwa ajili ya wakati Wake, likifanywa halisi na kuthibitishwa mbele zao ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Mjumbe wa wakati huo. Wala haikumlazimu kueleza jambo lo lote.

¹⁰⁹ Huenda hao wanafunzi wasingeweza kueleza jambo Hilo. Bali waliliamini, kama wangeweza kulielezea ama la. Walikaa kimya kabisa na kuliadini. Wangejua kama watakula mwili Wake na kuinywa Damu Yake? Mbona, wasingeweza kufanya jambo hilo. Lakini waliliamini, kwa maana walikuwa wamechaguliwa. Yesu alisema aliwachagua “kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.” Unaona? Waliadini. Kama waliweza kuelezea jambo hilo, ama hawangeweza, bado waliliamini.

¹¹⁰ Sasa angalia, Sasa, katika wakati wa saba wa kanisa, “Wakati malaika wa saba atakapoanza kutangaza, siri za Mungu zilipaswa kujulikana papo hapo,” Ile Mihuri.

Ambayo, wale watengenezaji ambao . . . kama wanalikuwa na wakati. Luther hakuishi muda mrefu vya kutosha, wala Wesley. Nyakati hizo hazikudumu muda mrefu vya kutosha, hao watengenezaji. Walikuwa na ujumbe wao wa siku hiyo, nao watu wakaushika na kuufanya madhehebu. Na ni kitu gani?

¹¹¹ Huwezi kushinda maumbile kamwe. Maumbile daima hushuhudia. Mungu huenda moja kwa moja pamoja na maumbile. Haina budi kuwa hivyo.

Kama vile jua. Jua linachomoza asubuhi, ni mtoto mchanga anayezaliwa. Ni nyonge, halina joto sana. Saa nne, linamaliza shule ya sekondari. Mchana, linaingia katika maisha. Saa tisa alasiri, linaanza kuzeheka. Saa kumi na moja, linaanza kufa, ni

zee na halina nguvu tena, linarudi kaburini. Je! huo ndio mwisho wake? Linachomoza tena, asubuhi inayofuata. Unaona?

¹¹² Angalia miti jinsi inavyootesha majani yao, kila kitu ifanyacho. Sasa tunaona, majani hupukutika kutoka mtini, yanarudi. Ni nini? Uhai unashuka unaenda kwenye mizizi ya mti huo. Huo ndio mwisho wake? Unarudi kwenye majira ya kuchipua, ukiwa na maisha mapya.

¹¹³ Sasa, angalia makanisa, jinsi yalivyofanya jambo lile lile katika yale matengenezo. Iliota. Ile chembe ya ngano ilianguka ardhini ikafa, chini ya yale mateso ya ule wakati wa giza. Iliingia ardhini. Ilibidi ife. Mtu ye yote, wa kiroho, anaweza kuona jambo hilo. Hiyo mbegu isipokufa na kuoza, inakaa peke yake. Na ilibidi iingie ardhini, chini ya ule wakati wa giza. Ilikaa humo, ikaoza. Kisha ikachipuka katika majani mawili ya kanisa la Kilutheri. Kutoka katika kanisa la Kilutheri, yakatokea majani mengine zaidi, Zwingli na kadhalika. Kutoka kwa hayo ikafikia kwenye kishada, ambacho kilikuwa ni John Wesley, ule wakati mkuu wa kimishenari. Ukarudi nyuma. Kutoka hapo ukaja ule wakati wa udanganyifu, ule wakati wa Kipentekoste. Ile punje ya ngano ambayo. . .

¹¹⁴ Je! kuna mtu ye yote, hapa, aliyepata kukuza ngano? Hebu angalia hiyo ngano utakapoiangalia. Unapotoka kwenda kule, unasema, “Nina ngano.” Inaonekana kana kwamba una ngano pale. Hebu ifungue kwa makini sana na uiangalie. Huna ngano hata kidogo. Una kapi. Je! Yesu hakutuonya hayo, katika Mathayo 23:22. . . nne? “Katika siku za mwisho roho hizo mbili zingefanana sana, hata ingeipoteza ngano yenyewe iliyoteuliwa kama yamkini.” Unaona? Sasa angalia, ni bebaji.

¹¹⁵ Sasa, Uhai uliotokea kupitia kwa Luther ndio uliomleta Wesley. Uhai uliotoka kwa Wesley ndio uliofanya Pentekoste. Uhai unaotoka katika Pentekoste ndio unaoifanya ile ngano. Bali hao ni wabebaji. Unaona? Ule uhai halisi hupitia pale. Ujumbe unapita, bali unaelekea moja kwa moja kwenye ngano. Hiyo ndiyo sababu ngano ilichipuka na kuleta kitu hicho kizima katika Kunyakuliwa, hapa juu kileleni. Bibi-arusi, Mwenyewe, anatoka kutoka katika kila wakati. Bali ubua wa kimadhehebu unakufa, unakauka na kufa. Umeisha gundua, siku hizi za mwisho, jinsi limeanza kujiondoa kwake sasa? Wakati ngano hiyo inapoanza kukua, ndipo ka—kapi linaanza kuachilia.

¹¹⁶ Rudi uangalie ndani ya maskini ngano hiyo unapoiangalia. Ifungue namna *hii*, na kuingalia ndani upate kuona. Unapata chipukizi dogo la ngano kule nyuma. Ingekulazimu kuchukua darubini ya kipimo cha thelathini kuiangalia ndani, upate kuona hicho kichipukizi cha ngano kule nyuma. Unaona?

Kiko kule nyuma ndani kabisa, lakini kinaanza kukua. Sasa, kapi hilo halina budi kuwapo, lipate kukifunika Hicho, ipate kukipa nafasi ya kutoka. Lakini basi kinapoanza kukua

na Ujumbe unaanza kusambaa, ndipo kapi hujiondoa kutoka kwacho. Ndipo Ule uhai unatoka moja kwa moja kwenye kapi hilo, unaingia moja kwa moja kwenye hiyo ngano. Unaendelea! Hivyo ndivyo kila wakati unavyofanya. Unaninii tu—hauwezi kuyashinda maumbile.Ni...Huo ni mwendeleo wa moja kwa moja wa Mungu, jinsi Yeye anavyotenda mambo.

¹¹⁷ Na sasa, huo ndio wakati tunaishi sasa hivi, wakati wa saba wa kanisa. Sasa, yote yatadhihirishwa katika hiyo punje ya ngano katika wakati wa mwisho, mwingine utakaorudi. Sasa, kama ukichukua Luka mlango wa 17 na kifungu cha 30, Yeye alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu, wakati Mwana wa Adamu atakapoanza kujifunua Mwenyewe.” *Kufunua* ni nini? Kufanya ufunuo wa vile Yeye alivyo katika siku hii. Afunuliwe, kwa watu, Neno ambalo limetambulishwa kwa ajili ya siku hiyo. Afunuliwe, kwa watu, kwa dhihirisho la Roho Mtakatifu akimfanya Yesu huyo kuishi miongoni mwetu. Na, kumbukeni, Yeye aliwakilishwa kule katika Mwanadamu. Mwanadamu! Alisema, “Kama ilivyokuwa...” Sasa, Yeye alisoma Biblia ile ile tunayosoma, Mwanzo. Sasa, tunaona katika ile sura ya Mwanzo pale, wakati Yesu alipokuwa akinena habari zake.

¹¹⁸ Tunaona pale, ya kwamba, katika jambo hilo, huku mgongo Wake umeelekezwa kwenye lile hema, na Sara akiwa hemani. Yeye alisema, aliuliza swali. Naye hakuamini kile kilichokuwa kitendeleo kingeweza kutendeka. Akasema, “Sasa, Ibrahimu, nitakuzuru wakati uu huu mwakani.” Unaona? Ndipo Sara, akiwa hemani, akacheka juu ya jambo hilo. Akasema, “Mbona Sara amecheka, huko hemani, akisema, ‘Mambo haya yanawezekanaje?’”

¹¹⁹ Yesu aliahidi. Na huyo alikuwa ni Yeye. Ibrahimu alimwita, “Elohimu,” Mwenyezi. Huyo alikuwa Ndiye. Sasa, Biblia inabashiri ya kwamba hilo litarudi tena katika siku za mwisho. Yesu alisema hivyo. “Na wakati mnapoona mambo haya yakianza kutimia,” kumbukeni tu, wakati jambo hili litakapoanza kutukia hivyo kama wakati huo, basi, “mnajua ya kwamba wakati uko karibu mlangoni.”

¹²⁰ Angalia ulimwengu wenyewe. Angalia ulimwengu, Sodoma, kama kulipata kuwako na Sodoma. Waangalie watu wamepotoka katika upotovu mkuu sana. Akili zao zimepotoka. Hawajui mwenendo mwema ni kitu gani. Angalia hawa wanyang’anyi...[Sehumu tupu kwenye kanda—Mh.]...uzinzi na kila kitu.

Pia waangalie wanawake wetu, jinsi walivyofanya ukatili. Angalia ni ukatili wa ukosefu wa uadilifu jinsi gani, uzinzi miongoni mwa wanawake wetu. Na si nani wetu tu... .

Unasema, “Hao ni Wamethodisti.” Hao ni Wapentekoste, pia. Ni kitu hicho chote.

¹²¹ Waangalie wanaume wetu. Wanashikilia, badala ya Neno la Mungu, mapokeo fulani madogo ya madhehebu. Wanayashikilia, badala ya kutoka wanapoona Mungu akijitambulisha kikamilifu sana. Sababu yake, wao ni vipofu. Hawawezi kuona jambo Hilo. Hawataliona kamwe.

Sasa, angalia kile kinachotendeka hapa katika jambo hili, tunapoharakisha.

Nafikiri yule bibi anataka tuondoke. Nimemwona akiashiria kwa mkono wake, kitu fulani kama kwamba anatutaka tutoke, kwa hiyo afadhali tuharakishe.

¹²² Kwa hiyo sasa mwangalie Henoko, mfano wa Kanisa. Hapa yeye anaonyeshwa kwa mfano pia katika wakati wa saba wa kanisa. Unaweza kuwazia jambo hilo? Wakati wa saba wa kanisa! Angalia. “Katika kutangaza kwa . . .”

¹²³ Ni wangapi wanaamini kumekuwa na wajumbe saba kwa jili ya ninii saba . . . Loo, sote tunaamini jambo hilo, kama tunaamini Biblia. Kama hatuamini Biblia, bila shaka, unaona, hatuliamini. Lakini, zimekuwako.

¹²⁴ Sasa hivi tunaishi katika wakati wa saba wa kanisa. Na wakati Biblia iliposema ya kwamba, wakati huu wa saba wa kanisa, “Wakati yule mjumbe wa wakati wa saba wa kanisa atakapoanza kutangaza Ujumbe wake, ya kwamba siri za mambo yote yaliyokuwa yamepotoshwa, katika hizo nyakati zote, yangefunuliwa katika wakati huo.” Hapa tunaona jambo hilo, Mwana wa Adamu akija miongoni mwa watu Wake na kufanya jinsi hiyo hasa, akithibitisha Ujumbe Wake kama alivyosema angefanya. Tupo hapa tunaona jambo hilo, katika wakati huu wa mwisho sasa.

¹²⁵ Na zile zamu saba, kama zile zamu saba, alikuja katika moja. Yeye hakuja katika zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, bali alikuja katika zamu ya saba. Huyu alikuwa ni Henoko, yule wa saba, ambaye alihamishwa. Ndipo Nuhu, akiwa ni mfano wa masalio ya Wayahudi, atavushwa apitishwe. Sasa, katika nyakati za Biblia, tukinena habari ya zile zamu. Na usiku haukugawanywa katika saa, katika wakati wa Biblia.

¹²⁶ Sasa sikilizeni kwa makini. Maana, nitaharakisha sasa, maana wanataka chumba hiki. La. Biblia haikugawanywa, ama—ama . . .

¹²⁷ Usiku haukugawanywa katika saa, katika wakati wa Biblia. uligawanywa katika zamu. Kulikuwa na zamu tatu. Sasa, zamu ya kwanza ilianza kutoka saa tatu hadi saa sita. Zamu ya pili ilianza kutoka saa sita mpaka saa tisa. Na zamu ya tatu ya usiku ilihesabiwa kutoka saa tisa mpaka saa kumi na mbili. Sasa tuna tatu, tatu-tatu, ambazo ni tisa, namba isiyokamilifu.

Ndipo tunarudi kwenye saba kwa ajili ya Kunyakuliwa, ambako kutatukia, naamini, kati ya saa saa kumi na mbili na saa moja . . . ama saa kumi na mbili na saa tatu, asubuhi fulani. “Kwa maana parapanda ya Bwana Italia.”

Katika asubuhi hiyo angavu na isiyo na mawingu wakati waliokufa katika Kristo watafufuka,
 Nao washiriki katika utukufu wa kufufuka Kwake;
 Wakati Wateule Wake watakapokusanyika manyumbani mwao ng'ambo ya mbingu,
 Majina yatakapoitwa kule ng'ambo, nitakuwako.

¹²⁸ Neno Kunyakuliwa, katika Biblia, hata halitumiki kabisa. Tumeliweka neno hilo tu pale. Biblia inasema, “Kutwaliwa; kutwaliwa.” Tunasoma hapa katika Wathesalonike wa Pili . . . Ama, ni Wathesalonike wa Kwanza, ndio utaratibu wa Kunyakuliwa huku kukuu ambako kutatukia katika siku za mwisho. Sikilizeni haya hapa. Tutaanzia hapa kwenye kifungu cha 13.

. . . ndugu, hatutaki msijue habari za hao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini.

Maana, . . . ikiwa twaamini ya kwamba Kristo alikufa akafufuka, vivyo hivyo . . . hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye.

Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia . . . (Ama neno hilo tangulia linamaanisha “kuzuia.”) . . . hao waliokwisha kulala mauti.

Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka . . .

Sasa, sikilizeni kwa makini.

. . . Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza . . .

¹²⁹ Nawatakeni muangalie jambo kubwa linalotukia hapa sasa. Msikose jambo hili. Mnaona? Sasa angalieni. Neno linasema hapa, katika Wathesalonike wa Pili, ya kwamba kuna mambo matatu. Angalia. Kutoka kifungu cha 13 mpaka cha 16, kuna mambo matatu ambayo hayana budi kutukia kabla Bwana Mwenyewe hajatokea. Upesi sasa, ili tuweze kufunga. Unaona? Jambo la kwanza linalotukia . . . Angalia: mwaliko, sauti, parapanda. Hebu na tulisome sasa tuone kama hilo ni kweli. Unaona?

*Kwa sababu Bwana mwenyewe... (kifungu cha 16)
atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti
ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu:...*

¹³⁰ Mambo matatu yanatukia. Sauti...mwaliko, sauti, parapanda, yanapaswa kutukia kabla ya kuonekana kwa Yesu. Sasa, mwaliko... Yesu anafanya yote matatu wakati Yeye ana—Yeye ana—Yeye ana—Yeye anaposhuka.

Mwaliko, mwaliko ni nini? Ni Ujumbe ukitangazwa, kwanza, kile Chakula cha Uzima kilicho hai kikimzaa Bibi-arusi.

¹³¹ Sasa, Mungu anayo njia ya kutenda mambo. Wala Yeye habadilishi mpango Wake. Kamwe Yeye habadilishi ninii Yake... Yeye ni Mungu asiyebadilika. Katika Amosi 3:7, Yeye alisema, “Asingefanya lo lote duniani mpaka kwanza alifunue kwa watumishi Wake manabii.” Na kwa hakika tu kama alivyoliahi, Yeye atalitimiza.

¹³² Sasa, tumepitia katika nyakati za kanisa. Lakini tumeahidiwa katika siku za mwisho, kulingana na Malaki 4, ya kwamba kutakuwako na kurudi tena, nabii nchini. Hiyo ni kweli. Angalia tabia yake, na jinsi atakavyokuwa. Yeye daima ni...

Mungu anamtumia roho huyo mara tano: wakati mmoja katika Eliya; katika Elisha; na katika Yohana Mbatizaji; kuliita Kanisa litoke; na masalio ya Wayahudi. Mara *tano*, “neema,” J-e-s-u-s, i-m-a-n-i, na ni namba ya neema. Unaona? Vema.

¹³³ Sasa, kumbuka, Ujumbe huo umeahidiwa. Na wakati siri hizi zote zimelundikwa na kundi la makasisi, itahitaji na—nabii wa moja kwa moja kutoka kwa Mungu atakayezifunua. Na hivyo ndivyo alivyoahidi kufanya hasa. Unaona?

¹³⁴ Sasa, kumbukeni, “Neno la Mungu humjia nabii,” si mwanatheolojia. Nabii, yeye ndiye mwakisi wa Neno la Mungu. Hawezi kusema kitu; hawezi kusema mawazo yake mwenyewe. Yeye anaweza kunena tu yale Mungu anayofunua. Hata kwa nabii Balaamu wakati alipojaribu kuuziwa—kuuza haki yake; yeye alisema, “Nabii ye yote anawezaje kusema neno lo lote ila lile Mungu analoweka katika kinywa chake?” Ni jambo ambalo Mungu anafanya, ambapo huwezi kusema jambo lingine. Nawe umezaliwa namna hiyo. Si zaidi ya vile ungeweza...

¹³⁵ Kama ungeweza kusema, “Si—si—siwezi kufungua macho yangu,” wakati unaangalia. Unaona? Huwezi. Huwezi kufikia mkono wako, wakati unaweza. Unaona? Huwezi kuwa mbwa wakati wewe ni mwanadamu. Unaona? Umeumbwa tu namna hiyo.

Na Mungu daima, pia, katika zile nyakati, kupitia kwa Isaya, Yereimia, na hao wote, Eliya, katika nyakati zilizopita. Wakati kundi la makasisi lingevuruga mambo yote, Yeye angemtuma nabii, amwinue kutoka mahali pasipo na maana.

Yeye hakuwa mfuasi wa hali zo zote zao, naye ananena Neno Lake. Akaondolewa jukwaani, na kutoweka, watu wagumu tu wa Ukweli wa Mungu. Na daima ndivyo tu ungeweza kumjua. Yeye alisema, “Kama kuna mtu wa kiroho miongoni mwenu ama nabii. . .”

¹³⁶ Sasa, manabii. Kuna kitu kama “karama ya unabii” Kanisani; bali nabii anachaguliwa tangu zamani na kuteuliwa tangu zamani kwa ajili ya wakati huo. Unaona? Naam, bwana. Sasa, kama unabii ukitokea, wawili ama watatu wanapaswa kuketi na kuamua kama hiyo ni kweli ama si kweli, kabla kanisa halijaupokea.

¹³⁷ Bali hakuna mtu anayewekwa mbele ya nabii, maana yeye alikuwa—alikuwa ni Neno la Mungu kabisa. Yeye alikuwa ndiye hilo Neno katika wakati wake. Alimwona Mungu akiakisi. Sasa, Mungu ameahidi kututumia huyo tena katika siku za mwisho, kumtoa Bibi-arusi kutoka kwenye hayo machafuko ya kidini, katika njia pekee linavyoweza kufanywa.

¹³⁸ Halitafanywa kamwe; kanisa haliwezi kumpokea Kristo. Sisi, Wapentekoste, hatuwezi kuubeba Ujumbe huu katika hali kanisa lilivyo siku hizi. Tutawezaje kuendeleza wakati wa mwisho katika hali waliyomo siku hizi, wakati kila mtu anampinga mwenziwe, na cho chote kile, na kidini? Loo, rehema! Ni machafuko. Limeingia katika madhehebu. Na wakati wo wote. . . ninamuuliza mwanahistoria ye yote ku—ku—kusema vinginevyo. Kila wakati ujumbe ulipotangazwa duniani, na wakati walipoufanya madhehebu, ulikufa papo hapo. Na Wapentekoste wamefanya jambo lile lile walilofanya hao wote, Wapentekoste waliotoka.

¹³⁹ Ninyi, Assemblies of God, wakati babu zenu na mama zenu walipotoka katika hayo madhehebu huko yuma, katika ile Halmashauri Kuu ya kale, wakipaza sauti na kumsifu Mungu, na wakapinga mambo hayo. Nanyi mkageuka, “kama mbwa kwenye matapiko yake, na nguruwe kwenye kugaa-gaa katika matope yake,” na mkafanya jambo lile lile walilofanya. Na sasa mko wa kidini sana, hivi kwamba mmefunga moyo wenu wa huruma. Inabidi uwe na kadi ya ushirika kabla ya mtu kuweza kushirikiana nanyi, ni vigumu.

¹⁴⁰ Ninyi, wa umoja, Mungu aliwapa ujumbe kama huo, na badala ya ninyi kuendelea, na kudumu wanyenyekevu tu na kusonga mbele, iliwabidi kulegea na kulifanya kundi lenu madhehebu. Basi ninyi nyote mko wapi? Kwenye ndoo ile ile. Hiyo ni kweli hasa.

Na Roho wa Mungu, akisonga mbele. “Mimi Bwana nitalipanda. Nnitalitia maji, mchana na usiku. Asije mtu. . .” Yeye aliamuru mambo haya yawe hivyo, Naye hana budi kumtuma Huyu.

¹⁴¹ Jambo la kwanza linalotukia, wakati Yeye anapoanza kushuka kutoka Mbinguni, kuna mwaliko. Ni kitu gani? Ni Ujumbe, wa kuwakusanya watu pamoja. Ujumbe unatokea, kwanza. Sasa, wakati wa kutengeneza taa, “Amkeni mkazitengeneze taa zenu.” Hiyo ilikuwa ni zamu gani? Ya saba, si ya sita. Ya saba, “Tazama, Bwana arusi yuaja. Amkeni mkazitengeneze taa zenu.” Nao wakaamka kuzitengeneza. Baadhi yao wakakuta kwamba hata hawakuwa na Mafuta yo yote katika taa zao. Unaona? Lakini ni wakati wa kutengeneza taa.

Ni wakati wa Malaki-4. Yale aliyoahi-... Ni Luka 17. Ni—ni Isa-... Nabii hizo zote ambazo Hilo linaweza kuwekwa katika utaratibu mkamilifu kuhusu siku hizi, katika Maandiko, tunaona jambo hili likiwa hai papo hapo. Hakuna...

¹⁴² Unaona mambo haya yakitukia, ndugu yangu mpendwa, dada. Wakati, Mungu Mbinguni anajua ningeweza kufa hapa jukwaani sasa hivi. M—mnapaswa tu kutembea huku na huku kwa muda kidogo. Ni ninii tu... Ni jambo kuu sana, unapomwona Mungu akishuka kutoka Mbinguni, anasimama mbele ya makundi ya watu, na kusimama pale, anajidhihirisha Mwenyewe kama tu vile alivyowahi kufanya. Na hiyo ni Kweli, na Biblia hii ikiwa imefunguliwa. Unaona? Kweli. Tumewasili.

¹⁴³ Na mfumo wa kimadhehebu umekufa. Umekwisha. Hautainuka tena. Utateketezwa. Hivyo ndivyo mnavyofanya na makapi shambani. Ukimbieni. Ingieni katika Kristo. Usiseme, “Mimi ni mfuasi wa Methodisti. Mimi ni mfuasi wa Baptisti. Mimi ni mfuasi wa Pentekoste.” Wewe ingia katika Kristo.

Kama wewe umo ndani ya Kristo, hakuna neno lililoandikwa ndani hapa ila lile unaloamini. Sijali vile mtu mwingine ye yote alivyosema. Ndipo basi Mungu anapofanya jambo hilo lidhihirishwe. Maana, wewe, wakati Yeye anapomwaga Roho juu ya Neno, ni jambo gani linalotukia? Ni kama tu kutia maji juu ya mbegu nyingine yo yote. Itaishi, na itazaa ya jinsi yake.

¹⁴⁴ Unasema, “Nilipata ubatizo, Roho Mtakatifu.” Hilo halimaanishi ya kwamba umeokoka, yanaachana kwa mbali sana.

¹⁴⁵ Angalia hapa. Wewe ni kiumbe cha utatu. Ndivyo ulivyo. Ndani ya jamaa *huyu* mdogo hapa kuna nafsi, inayofuata ni roho, na hiyo nyingine ni mwili. Sasa, una hisi tano katika mwili huu, za kuwasiliana na makazi yako ya duniani. Haziwasiliani na huko kwingine. Una hisi tano za roho, *hapa*: upendo na dhamira, na kadhalika, za hiyo. Lakini *hapa* ndani ndipo *wewe* unapoishi. Hivyo ndivyo ulivyo.

¹⁴⁶ Je! Yesu hakusema, “Mvua huwanyea wenye haki na wasio haki”? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hebu weka gugu hapa nje, na ngano huko nje, kisha uzimwagie maji, na uzidumishe kwa mbolea na vitu kama hivyo, zote si zitaishi kwa

maji yale yale? [“Amina.”] Hakika. Vema, ni kitu gani? Moja itazaa gugu, kwa kuwa hivyo ndivyo tu ilivyo. Gugu litainua mikono yake na kupiga makelele vile vile tu kama ngano.

¹⁴⁷ Je! Biblia haikusema, “Katika siku za mwisho, watakuja Makristo wa uongo”? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Sio “Mayesu wa uongo,” sasa. “Makristo wa uongo,” waliopakwa mafuta, waliopakwa mafuta wa uongo kwa Neno; wamepakwa mafuta kimadhehebu, bali si kwa Neno.

Kwa kuwa, Neno litajishuhudia Lenyewe. Halihitaji kitu kingine cho chote. Litajishuhudia Lenyewe.

“Na watatokea wapakwa mafuta wa uongo.” Mna kanda yangu juu ya jambo hilo. Na hao wapa- . . .

Loo, kama ungeweza kumwita mmoja wao, useme, “Loo wewe—wewe ni Yesu?”

“Loo, bila shaka hapana.” Wasingevumilia jambo hilo.

¹⁴⁸ Lakini inapofikia kwenye, “Ee utukufu! Nina upako!” Na ni upako wa kweli. Kumbukeni, Kayafa alikuwa Nao, pia, na akatabiri. Vivyo hivyo na Balaamu alikuwa Nao, na akatabiri.

Lakini hilo halina uhusiano wo wote na *hili*, la ndani. Isipokuwa hiyo iwe ilikuwa ni mbegu ya Mungu, jeni Yake tangu mwanzo, iliyokusudiwa tangu zamani, umekwisha. Sijali unapiga makelele jinsi gani, unavyonena kwa lugha, kukimbia, kupiga makelele. Hilo halina uhusiano wo wote na jambo hilo.

Gugu linaweza kuonekana jinsi ile ile kama hao wengine. Nimeona makafikiri wakiinuka, na kupiga makelele, na kunena kwa lugha, na—na kunywa damu kutoka katika fuvu la kichwa cha mwanadamu, na kumwita Ibilisi. Unaona? Kwa hiyo huninii . . . Yo yote ya mihemko hiyo na kadhalika; yasahau.

Ni moyo wako katika hilo Neno, na huyo ni Kristo. Liingize ndani pale, na uone likijitambulisha Lenyewe, linapofunguka tu kama mbegu nyingine yo yote, na kujitangaza Lenyewe kwa wakati linaoishi.

¹⁴⁹ Luther hangaliweza kuleta cho chote ila vichipukizi. Hawa wengine wangeweza kuleta mambo haya mengine. Tuko katika wakati wa ngano sasa.

Walutheri halisi wa Waluther iliwabidi kumzaa Luther halisi. Mpentekoste halisi ilibidi azae Pentekoste halisi. Hivyo tu. Lakini tumepita wakati huo, na tunaendelea.

¹⁵⁰ Je! mnajua, kanisa Katoliki, lilianza, likiwa la Kipentekoste? Na kama kanisa la Kipentekoste lingedumu kwa muda wa miaka elfu mbili, lingekuwa katika hali mbaya zaidi kuliko Katoliki lilivyo sasa. Hiyo ni kweli kabisa. Ninasema jambo hilo kwa ndugu zangu, dada zangu ninaowapenda. Na Mungu anajua jambo hilo. Lakini kumbukeni, enyi marafiki, sina budi kukutana nanyi huko ng'ambo kwenye ile Hukumu. Na hiyo

huenda isiwe ni muda mrefu sana. Sina budi kushuhudia ile Kweli.

¹⁵¹ Nilipotoka nikaenda kwenye mikutano pamoja nanyi, nikiwaombea wagonjwa, ilikuwa ni sawa. Walakini, nilipokuja na Ujumbe! Kama ujumbe wo wote ukitolewa, kama ni ujumbe wa kweli. . .

Kama ni miujiza ya halisi, ya kweli ya Mungu, na mtu aendelee kukaa katika madhehebu hayo, basi unajua si wa Mungu, maana jambo hilo limetangazwa tayari.

Yesu alitoka akaenda akawaponya wagonjwa, kusudi apate kuyavuita macho yao, hao watu, kisha alete Ujumbe Wake. Hiyo ni kweli.

Hapana budi pawe na jambo ambalo Mungu ataleta. Yeye ananinii tu. . . Kuponya Kiungu, miujiza Yake kama hiyo, ni kwa ajili ya kuvutia tu macho ya watu. Kiini cha jambo lenyewe ni ule Ujumbe. Hivyo ndivyo ilivyo, kile kinachotoka kutoka *hapa* ndani. Yeye anajaribu kupata kibali cha watu, wapate kuketi na kumsikiliza Yeye, unaona, kwa kuwa kuna wengine mle ndani waliokusudiwa Uzima.

Baadhi ya punje, ngano, ilianguka ardhini, na ndege wakaiokota. Na nyingine zilianguka katika miiba. Na nyingine zilikuwa, zilienda kwenye udongo uliotayarishwa, udongo uliotayarishwa awali, na zikazaa.

¹⁵² Sasa, ni jambo la kwanza, ni kule kutangazwa. Kitu cha kwanza ni parapanda na ninii. . . ama sauti. . . Mwaliko; na halafu sauti, na halafu parapanda.

Mwaliko: mjumbe akiwatayarisha watu.

La pili ni sauti ya ufufuo: sauti ile ile, ambayo, sauti kuu katika Yohana Mtakatifu 11:38-44, iliyomwita Lazaro kutoka kaburini.

Kumkusanya Bibi-arusi; na baadaye ufufuo wa wafu, unaona, apate kutwaliwa pamoja Nayo. Sasa angalia hayo mambo matatu yakitukia. Jambo lililofuata ni nini? Ilikuwa ni parapanda. Sauti. . . mwaliko; sauti; parapanda.

¹⁵³ Sasa, jambo la tatu, ni parapanda. Ambayo, daima, kwenye Sikukuu ya Baragumu, inawaita watu kwenye karamu. Na hiyo itakuwa ni Karamu ya Bibi-arusi, Karamu ya Mwana-Kondoo pamoja na Bibi-arusi, huko hewani. Unaona?

¹⁵⁴ Kitu cha kwanza kutokea ni Ujumbe Wake, ukimkusanya Bibi-arusi. Jambo la pili ni kufufuliwa kwa Bibi-arusi aliyelala; wale—wale waliokufa, huko nyuma katika zile nyakati nyingine, wanatwaliwa pamoja. Na parapanda, ile karamu ya mbinguni, hewani. Mbona, hilo ndilo jambo linalotukia, enyi marafiki.

¹⁵⁵ Tuko papo hapo kabisa, tayari sasa. Jambo pekee, Kanisa linalotoka, halina budi kukaa mbele za Mwana, lipate kuivishwa.

Kile kivuna nafaka kikuu kitakuja, muda si muda. Ngano itachomwa moto, yale mashina, bali ngano itakusanywa katika ghala Lake. Unaona?

¹⁵⁶ Ninyi si vipofu. Ninyi—ninyi ni watu wenye akili.

Na kama nilisimama hapa na kusema mambo hayo kwa upendeleo? Ninayasema kwa sababu ni Uzima, kwa maana mimi ninawajibika kwa Mungu kwa kusema Hilo. Nami sina budi kulisema, Na Ujumbe wangu. Wakati wote, nikijua, kule nyuma chini ya uponyaji na kadhalika namna hiyo, ilikuwa tu ni kwa ajili ya kuvutia usikivu wa watu, nikijua Ujumbe utakuja. Na ndio huu hapa. Na hiyo Mihuri Saba ilifunguliwa, siri hizo, na kuonyesha mambo hayo ndiyo yalilotukia. Mimi sikujua hayo.

¹⁵⁷ Lakini wapo watu wanaosimama papa hapa sasa, waliokuwa wamesimama papo hapo pamoja nami. Wakati, ninyi nyote mlinisikia nikihubiri Ujumbe ule: *Mabwana, Ni Wakati Gani?* Asubuhi hiyo, mahali papo hapo iliposemwa itatukia, papo hapo walisimama wale Malaika Saba, kutoka Mbinguni. Nao walipokuwa wakipaa juu, na huo upepo wa kisulisuli ukawapeleka kule juu, sisi tukiwa tumesimama, tukiangalia walipokuwa wakienda zao, sayansi ilipiga picha Yake, kote nchini, hadi huko Mexico.

¹⁵⁸ Na hapo, wakati nilipokuwa nikiangalia, siku moja wakati nilipoanza kuhubiri hizi *Nyakati Saba za Kanisa*, Basi nilimwita Jack Moore, mwanatheolojia mashuhuri. Nikasema, “Jack, Mtu Huyu ni nani ambaye anasimama pale? ‘Kuna Mtu kama Mwana wa Adamu amesimama pale, nywele nyeupe kama sufu.’” Nikasema, “Yeye alikuwa ni kijana Mwanamume, angeweza kuwa na nywele nyeupe kama sufu?”

¹⁵⁹ Akasema, “Ndugu Branham, huo ulikuwa ni mwili Wake uliotukuzwa.” Hilo halikugonga moyoni.

Lakini nilipoingia chumbani na kuanza kuomba, Yeye alinipa kujua ilikuwa ni nini. Unaona?

¹⁶⁰ Daima nimehubiri ya kwamba Yeye alikuwa ni Mungu, si mwanadamu tu. Alikuwa ni Mungu alivyodhihirishwa katika mwili: Mungu, sifa za Mungu, za upendo; zile sifa kuu za Mungu, zilizoshuka, zikionyeshwa hapa duniani. Yesu alikuwa ni upendo wa Mungu, ambao aliumba mwili ambamo Yehova Mwenyewe aliishi. Yeye alikuwa ni utimilifu wa Mungu kwa jinsi ya mwili. Yale Mungu aliyokuwa, Yeye aliyadhihirisha kupitia katika mwili huo. Ilibidi mwili huo ufe, kusudi Yeye apate kumwosha Bibi-arusi kwa ninii Yake—kwa ninii Yake—kwa Damu Yake.

¹⁶¹ Basi angalia, si kwamba tu Bibi-arusi ameoshwa, amesamehewa, bali amehesabiwa haki. Unaona? Je! ulipata kujaribu neno *kuhesabia haki*, kuona linavyoamaanisha?

Sasa, kwa mfano, kama Ndugu Green alisikia ya kwamba nilikuwa nikinywa pombe, nimekuwa nikifanya mambo mabaya,

halafu akakuta kwamba sikuyafanya. Ndipo aje, aseme, “Ninakusamehe, Ndugu Branham.”

¹⁶² “Ati unanisamehe? Mimi sijawahi kufanya jambo hilo. Unanisamehe kitu gani?” Unaona? Bali kama nina hatia, basi ninaweza kusamehewa; bali ningali sina haki, kwa maana nilifanya jambo hilo.

Lakini neno *kuhesabiwa haki* ni “kana kwamba hujapata kufanya jambo hilo, kamwe.” Kuhesabiwa haki! Ndipo Damu ya Yesu Kristo inatusafisha na dhambi, mpaka inawekwa katika Kitabu cha usahaulifu wa Mungu. Yeye ndiye pekee anayeweza kufanya jambo hilo.

¹⁶³ Sisi hatuwezi. Tunaweza kusamehe, bali si kusahau. Ningeweza kukusamehe, bali daima nitakumbuka ulifanya mambo haya mabaya. Ndipo, wewe si mwenye haki; umesamehewa.

Lakini, mbele za macho ya Mungu, Bibi-arusi amehesabiwa haki. Kwanza kabisa, hakupata kufanya hilo. Amina. Amesimama pale, ameoledwa na Mwana mtakatifu wa Mungu; jambo la kwanza, hajawahi kamwe kufanya dhambi. Kwa nini? Yeye alichaguliwa tangu zamani. Aliingizwa kwenye mtego huu. Na sasa wakati alipoisikia ile Kweli na akatoka, ile Damu ilimsafisha. Naye anasimama pale, akiwa mtakatifu. Unaona? Yeye, hana dhambi, hata kidogo.

¹⁶⁴ Kwa hiyo, Ujumbe unamkusanya Bibi-arusi, unaona, ule mwaliko.

Na parapanda . . .

Ile ile, Yeye, kwa sauti kuu, Yeye alipaza sauti kwa mwaliko huo na sauti, na kumwamsha Lazaro. Yeye alisema kwa sauti kuu, “Lazaro, njoo huku.” Unaona? Na sauti hiyo inamwamsha—inamwamsha Bibi-arusi aliyelala, wafu waliolala mauti.

¹⁶⁵ Na ile parapanda, “kwa sauti ya parapanda.” Na, wakati itakapolia, inaita. Daima, parapanda iliwaita Israeli kwenye sikukuu ya baragumu. Unaona? Ambayo, ilikuwa ni Sikukuu ya pentekoste, ile Sikukuu kubwa hewani; na sikukuu ya baragumu. Na, sasa, baragumu ilimaanisha kuita watu pamoja, “Njoni kwenye Karamu.” Na sasa hiyo Ka—Karamu ya Mwana-Kondoo hewani.

Sasa, angalia. Kukusanyika pamoja; na Bibi-arusi; karamu ya baragumu, ile Karamu ya Arusi. Tumeiona katika mifano. Sasa hebu angalieni kwa muda kidogo tu kabla hatujafunga. Angalia. Tumeiona katika mifano.

¹⁶⁶ Sasa, kama unataka kusoma katika Mathayo 18:16, ilisema, “Wako watatu wanaoshuhudia,” unaona, katika Yohana Mtakatifu . . . katika Yohana wa Kwanza 5:7, na kadhalika. Daima tatu ni shahidi. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni thibitisho, jambo fulani ambalo ni

kweli. Mashahidi watatu wanashuhudia. “Katika kinywa cha mashahidi wawili ama watatu, kila neno lithibitike.”

¹⁶⁷ Sasa angalia. Tumekuwa na mashahidi watatu. Tatu ni shahidi. Sasa, tayari tumekuwa na kunyakuliwa kutatu katika Agano la Kale. Je! ulijua jambo hilo? Kama shahidi. Sasa angalia. Henoko alikuwa mmoja wao; Eliya alikuwa huyo mwingine; na Yesu Huyo mwingine.

Yesu, akiwa ndiye Jiwe la Katikati, sasa, Yeye alishuhudia. Unaona? Yeye alikuwa ndiye Jiwe la Katikati kati ya Agano la Kale na Agano Jipya, kwa maana ilimpasa Yeye kwanza kufa halafu kunyakuliwa. Yeye alikufa; akafufuka kisha akatembea hapa pamoja nasi; na kisha akanyakuliwa. Kwa kuwa, Yeye alikuwa ni Jiwe la Katikati lililounganisha kunyakuliwa kote kuwili pamoja. Baada ya kufufuka Kwake na kunyakuliwa... Angalia. Baada ya Yeye kufanya jambo hilo, na kuthibitisha hilo, Agano la Kale pale. Sote tunajua Henoko aliamishwa. Tunajua Eliya alitwaliwa na upepo wa kisulisuli, hiyo ni kweli, katika gari la moto. Naye Yesu alikufa, akazikwa, akafufuka na kuishi hapa duniani, na kisha akanyakuliwa, lile Jiwe la Katikati. Kuna hao watatu, wa kushuhudia. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

¹⁶⁸ Sasa, kumekuwako na kunyakuliwa kumoja ambako kumepita tayari. Je! ulijua jambo hilo? Huko, hebu tuone kama hatuwezi kukusoma, upesi sana. Hebu na tufungue Mathayo, mlango wa 27. Na hebu tufungue kwenye kifungu cha 45 cha Mathayo, mlango wa 27. Hebu tuone kama hatuwezi kupata jambo hilo upesi sana, na tuone kama—kama hatuwezi kupata kidogo tu kutoka katika hiki, kingetusaidia, upesi sana. 27:45, ninaamini nimeliandika hapa. Hebu tusome.

Basi tangu saa sita palikuwa na giza juu ya nchi yote mpaka saa tisa...

Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akisema, Eloi, Eloi, lama sabak...? yaani, Mungu wangu, ...mbona umeniacha?

Na baadhi yao waliohudhuria,...-liposikia, walisema, Huyu amwita Eliya.

Mara mmoja wao akaenda mbio, akatwaa sifongo, akaijaza siki, akaitia juu ya mwanzi, akamnywesha.

Wale wengine wakasema,...na tuone kama Eliya anakuja na kumwoko.

Naye Yesu akiisha kupaza sauti...kwa nguvu, akaitoa...

“Kupaza sauti.” Sauti kubwa! Angalia.

Wakati Yesu, akifa, alipaza sauti, akaitoa roho yake.

Na tazama, pazia la hekalu likapasuka vipande viwili toka juu hata chini; nchi ikatetemeka; miamba ikapasuka;

Makaburi yakafunuka; ikainuka miili mingi... watakatifu waliolala;

Nao wakiisha kutoka makaburini mwao, baada ya kufufuka kwake, wakauingia mji mtakatifu, wakawatokea wengi.

169 Kunyakuliwa kumoja kumepita.

Kutatu kumetukia katika Agano la Kale, kwa wale waliokuwa wamewekwa tayari, ambao walijiliwa na Neno la Bwana. Unaona? Neno la Bwana lilimjia Henoko. Neno la Bwana lilimjia Eliya. Yeye alikuwa ni nabii. Unaona? Neno la Bwana lilikuwa ni Yesu. Unaona?

170 Angalia katika Agano la Kale, hao watakatifu wa Agano la Kale sasa, wakati kunyakuliwa huku kulipotukia kwa mara ya kwanza. Angalia kifungu cha 50. Sauti Yake kuu iliwafulua watakatifu wa Agano la Kale kama tu vile hasa ile sauti kuu ilivyomwamsha Yesu... ama ilivyomwamsha Lazaro. Unaona? Sauti kuu ilifufua.

Na kwa pili kunatimizwa katika Wathesalonike wa Pili, mlango wa 4. Hebu na tusome tu, tulisome. Hivi punde tu tumepasoma dakika chache zilizopita. Unaona?

“Sitaki msijue, ndugu, habari za wao waliolala mauti, msije mkahuzunika, kama...”

Hiyo ni Wathesalonike wa Kwanza 4:12-18. Huko, huko kutakuwa ni Kunyakuliwa kwa pili. Kunyakuliwa kwa pili kutakuwa ni kuhamishwa kwa Bibi-arusi.

171 Watakatifu wa Agano la Kale wameenda mbele ya Uwepo Wake, peponi imeondolewa. Na watakatifu wa Agano la Kale walipaa juu, wakati wa sauti Yake kuu, wakati alipopaza sauti na kutoa roho; kwa sababu (gani?) Ile Dhabihu, msamaha wa dhambi zao, ambao walikuwa wameungojea, wakiamini ya kwamba huyo Mwana-Kondoo mkamilifu alikuwa anakuja. Walikuwa wametoa Dhabihu, yule Mwana-Kondoo. Na wakati Yeye alipokufa na kutoa roho Yake, Yeye alilia kwa sauti kuu, nao watakatifu wa Agano la Kale wakaamka.

Angalia ule mwaliko na ile sauti hapa, ni jambo lile lile wakati wa Kuja Kwake. Unaona?

“Akatoa roho Yake.” Na wakati alipofanya hivyo, ile dhabihu ikawa imekamili, ndipo peponi kukawa tupu. Nao watakatifu wa Agano la Kale wakaja duniani tena, wakatembea duniani, kisha wakaingia pamoja Naye, katika kunyakuliwa Kwake.

172 Daudi alisema, pale, “Inukeni, enyi malango ya milele, na inukeni.” “Aliteka mateka, akawapa wanadamu vipawa.” Wakati watakatifu wa Agano la Kale walipoingia pamoja Naye.

173 Walisema, “Ni nani huyu Mfalme wa haki?”

174 “Bwana wa Utukufu, mwenye nguvu katika jeshi.” Majeshi yenye nguvu, haya hapa yanaingia, yakitembea kiaskari. “Yesu aliteka mateka,” Naye huyu hapa anakuja, pamoja na watakatifu wa Agano la Kale. Ndipo akaingia katika malango mapya kule Juu, na kusema, “Inukeni, enyi malango ya milele, inukeni. Na Mfalme wa Utukufu apate kuingia.”

Sauti ikatoka upande wa ndani, ikasema, “Ni nani huyu Mfalme wa utukufu?”

175 “Bwana, hodari wa vita.” Malango yakafunguka mara moja. “Ndipo Yesu, aliye Mshindi, akateka mateka,” hao waliokuwa wamemwamini Yeye, nalo Neno lilikuwa limewajia. Hao hapo, watakatifu wa Agano la Kale wamekaa pale, wanangoja. “Aliteka mateka; akapaa Juu,” akawachukua watakatifu wa Agano la Kale na kuingia. Huko hapo Kunyakuliwa kumoja, kumepita tayari.

176 Kunyakuliwa kwa pili kunakotukia ni Wathesalonike wa Pili kwa ajili ya Kanisa, Bibi-arusi atakayefufuliwa, apate kunyakuliwa aingine katika Utukufu. “Sisi tulio hai na tutakaosalia,” hiyo ni miili iliyoachwa hapa duniani, “hatutawatangulia ama kuwazuia hao waliokwisha kulala mauti. Kwa maana parapanda ya Mungu italia kwanza, nao waliokufa katika Kristo watafufuka.” Unaona? “Nasi tulio hai na tutakaosalia tutanyakuliwa pamoja nao.”

177 Hivi majuzi, nilikuwa nimesimama kando pembeni mwa barabara. Nami ni—nilikuwa nimesimama kwenye... nilikuwa nimesimama pembeni mwa barabara nikiangalia gwaride la Sikukuu ya Kusimamisha Vita, na wakati walipopanda, wakipanda kwenda barabarani. Nilisimama pale pamoja mwanangu mdogo, Joseph. Vikaja, vya kwanza kupita, vilikuwa ni vifaruu vya kale vya vita vya kwanza, maskini vifaruu vidogo vya kale. Baada ya hivyo vikaja vifaruu vikubwa vya Sherman vya vita vipya, na mizinga yao mikubwa pamoja na mitutu yao ya kulipulia, vi—vyenye vivunja mtutu, na kadhalika.

Baadaye, wakaja askari; a—a—akina mama wa Nyota ya Dhahabu. Ndipo likaja gari lenye jukwaa pamoja na... na kuendelea... Vema, moja kwa moja kule nyuma likaja gari lenye jukwaa, na mbele yake palikuwa na kaburi, “kwa askari asiyejulikana.” Na hapo alisimama a—askari amesimama pale, akilinda kaburi hilo. Palisimama askari wa manowari upande huo mwingine, na baharia upande huo mwingine. Na kulikuwako na mgawanyo. Na upande huo mwingine alisimama mama mwenye Nyota ya Dhahabu. Alikuwa amempoteza mvulana wake. Pale alisimama mke mchanga amelaza kichwa chake mezani, analia. Maskini mvulana mmoja mwenye nguo zilizochakaa ameketi kwa upande; na machozi yakimtiririka usoni mwake. Alikuwa amempoteza baba yake.

Nikawazia, “Ni huzuni jinsi gani! ninasimama hapa na kuangalia, ninawaona hao, wazee, askari wachache tu waliosalia; wakitembea kule chini, wametiwa kilema na wamezeeka, namna hiyo, wamevaa nguo zao rasmi, lakini wakizionesha kwa fahari, kwa kuwa wao walikuwa ni Wamarekani.”

Nikawaza, “Ee, Mungu wangu!”

¹⁷⁸ Siku moja, kutakuja mlipuko kutoka Mbinguni, “Na waliokufa katika Kristo watafufuka kwanza.” Hao watakatifu wa Agano la kale kule nyuma, wanaongojea, watafyatuka na watoke huko kwanza, waingie katika ufufuo. Tutaingia moja kwa moja mstarini, na kwenda hewani; miili hii ya kale inayopatikana na mauti itabadilishwa na kufanywa kama mwili Wake wa utukufu. Litakuwa ni gwaride la jinsi—jinsi gani wakati litakapoanza kuelekea mbinguni, moja ya siku hizi, katika wakati huo wa kunyakuliwa ulio mbele yetu, loo, wakionesha kwa fahari Damu ya Yesu Kristo vifuani mwao, Ujumbe wa Mungu katika majira waliyoishi. Hiyo ndiyo saa tunayoitarajia, ndugu.

¹⁷⁹ Angalia, katika kufunga tu sasa. Ufufuo wa pili, wote... wa Kwanza umepita. Wa pili umekaribia, sasa hivi, utakuja kutimia sasa.

¹⁸⁰ Sasa, wa tatu ni wale mashahidi wawili wa Ufunuo 11:11 na 12. Ambao, hawa ndio wale wanaorudi, wakiwa na Roho wa Kristo, kuwashuhudia Wayahudi, kama vile Yusufu alivyofanya kwa ndugu zake. Nanyi kumbukeni, “Miili yao iliyokufa ilikaa katika njia ya mji, kwa muda wa siku tatu na nusu. Ndipo roho wa uhai akaingia ndani yao, nao wakanyakuliwa, wakapelekwa Mbinguni.”

Huko hapo kunyakuliwa kwenu kutatu kwa Agano Jipya.

Kunyakuliwa kutatu kwa Agano la Kale; kote kumepita.

¹⁸¹ Sasa tuko tayari, tuingojea nyakuo, Kunyakuliwa kwa watakatifu. Kumenenwa na hivyo basi kutatukia. Mungu anaposema jambo lo lote, “Mbingu zote na nchi zitapita, bali Neno hilo halitashindwa kamwe.”

¹⁸² Wakati Mungu aliposema, kule nyuma katika Mwanzo 1, alisema, “Iwe nuru.” Huenda palikuwa na mamia ya miaka kabla hakujakuwako na nuru yo yote. Alisema, “Na kuwe na mtende. Na kuwe na mwaloni. Na kuwe na jangwa. Na kuwa na mlima. Na kuwe ha *hiki*.” Yeye alitamka jambo hilo, unaona. Na mradi tu lilitoka katika kinywa Chake, katika Neno, halina budi kudhihirishwa. Lazima lidhihirishwe. Wakati...

¹⁸³ Ndipo siku moja, Yeye aliwaita watu Wake watoke. Naye alikuwa amenena na mtu mmoja jina lake Musa, kwa Nguzo ya Moto, Nuru; Moto mtakatifu, wenye Utukufu. Naye Musa

asingeninii...Watu wasingemwamini Musa, kwa hiyo Yeye akasema, “Walete kwenye mlima huu.”

¹⁸⁴ Asubuhi hiyo, ule mlima ulijaa Moto, na radi na ngurumo namna hiyo. Nao watu hao wakasema, “Usiache Mungu anene. Acha Musa anene, unaona, tusije tukaangamia.”

¹⁸⁵ Mungu akasema, “Sitanena nao tena namna hii, lakini nitawainulia nabii. Nami nitanena kupitia kwake, na asemalo litatimia. Basi, lisikilizeni, kwa kuwa Mimi—Mimi niko pamoja naye.” Sasa, Yeye alinena jambo hilo. Alisema ya kwamba litatimia.

¹⁸⁶ Mwangalie huyu nabii, Isaya, amesimama pale; mwanamume, mtu mwenye akili, mtu aliyeheshimika, vizuri, mbele ya mfalme, maana alikuwa ameishi pamoja na Uzia. Huyu mfalme, ambaye alikuwa ni mtu mashuhuri, alijaribu kupachukua mahali pa mhubiri, wakati mmoja, na akaingia, akapigwa kwa ukoma.

Na hivyo ndivyo nilivyowaambia hao wafanyabiashara. Msijaribu kamwe kupachukua mahali pa mhubiri. La, bwana. Kaa papo hapo mahali ulipo. Unaona? Fanya kazi yako, ile Mungu aliyoweka, aliyokwambia ufanye. Kama wewe ni kidole, huwezi kamwe kuwa sikio. Kama wewe ni sikio, hautakuwa pua kamwe, pua wala jicho. Unaona? Wewe kaa katika nafasi yako.

¹⁸⁷ Mlisikia Ujumbe huo, hivi majuzi, kwenye matangazo: *Kujaribu Kumfanyia Mungu Kazi*. Daudi, mfalme alyetiwa mafuta. Watu wote wakipiga makelele na kupaza sauti, “Tlikuwa ni sawa.” Bali yeye kamwe hakumtaka shauri nabii wa Mungu. Ndipo mtu akafa, na jambo zima lili vurugika. Usijaribu kumsaidia Mungu. Wewe ngojea mpaka muda wa Mungu utakapotimia. Acha jambo hilo lije katika njia Yake ya kulifanya jambo hilo. “Nitaanzisha jambo *hili* kubwa. Litafanya *hivi*.” Uwe mwangalifu, ndugu.

¹⁸⁸ Sasa, Daudi alijua ni vizuri kutokufanya hilo. Nathani alikuwa nchini, siku hizo. Hata hakutakwa shauri, kamwe. Unaona? Yeye aliwataka shauri maakida wa mamia na maelfu. Watu wote walipiga makelele, na kupaza sauti, na kucheza. Badala ya... Walikuwa na mihemko yote ya kidini, bali haikuwa katika mwelekeo na utaratibu wa Neno la Mungu, ndipo likakwama.

Jambo lo lote lile, lisilo katika utaratibu na mpangilio wa Neno la Mungu, litashindwa. Neno la Mungu ndilo tu litakalosimama milele. “Mbingu na nchi zitapita, bali si Neno Langu.”

¹⁸⁹ Angalia Isaya, kijana mwanamume huyo mwenye akili amesimama pale. Mara, Roho akamshukia. Hakuweza kutamka vinginevyo. Yeye alikuwa nabii. Akasema, “Tazama, bikira atachukua mimba.” “Kwa ajili yetu Mtoto amezaliwa; Mtoto amezaliwa, tumepewa mtoto Mwanamume. Ataitwa Jina Lake

Mshauri, Mfalme wa amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele. Mwisho wa... Uweza wa Kifalme utakuwa mabegani Mwake. Mwisho wa... Utawala Wake hautakuwa na mwisho." Mtu huyo angeweza kusema kwa akili ya kwamba bikira atazaa mwana?

Kila mtu alitarajia kuona jambo hilo. Limenenwa tayari. Lilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI. Ilibidi litimie, maana lilikuwa ni Neno la Mungu. Kama vile ilivyokuwa katika Mwanzo, wakati Yeye alipopanda hizo mbegu chini ya bahari, wakati "kulipokuwa ukiwa na tena utupu, na maji juu ya vilindi vya maji." Unaona? Ilibidi litimie. Ndipo siku moja, miaka mia nane baadaye, tumbo la uzazi la bikira likazaa Uzao wa Mungu, Uzao uliumbwa. Akamzaa Mwana.

¹⁹⁰ Mwana yuyo huyo alisimama pale, siku moja. Akasema, "Lazaro, njoo huku." Na mtu ambaye alikuwa amekufa siku nne, ameoza, pua yake imedidimia, alinuka; akatokea. Kasema,

"Msishangazwe na jambo hili, kwa maana saa yaja, amina, hapo wote walio kaburini watasikia sauti ya Mwana wa Mungu."

Kwa hiyo basi, limenenwa tayari. Halina budi kutukia namna hiyo. Kutakuwako na Unyakuo. Loo, jamani!

¹⁹¹ Ndio kwanza nikumbuke, ujumbe wangu wa mwisho huko California, ambako nilifikiri sitarudi tena, wakati nilipobashiri, "Los Angeles itazama chini ya bahari. Na BWANA ASEMA HIVI." Itazama. Imekwisha. Imeoshwa. Imekwisha. Wakati gani? Sijui ni lini, bali itazamishwa. Mara baadaye, matetemeko ya ardhi yakaanza kutikisa na kutetemesha.

¹⁹² Mnakumbuka, wengi wenu ninyi watu mkisimama pale pale, ule mwamba, siku ile wakati yule Malaika aliposhuka pale. Na ile Nuru na Moto ukishuka kutoka Mbinguni, kuzunguka mwamba ule wakati tulipokuwa tumesimama pale. Miamba ikirushwa kutoka mlimani, na kuanguka kule upande wa pili. Nalo lililipuka, kwa nguvu, mara tatu. Nikasema, "Hukumu itaipiga Pwani ya Magharibi." Siku mbili baada ya hayo, Alaska nusura izame.

¹⁹³ Kumbukeni, Mungu yeye yule aliyesema jambo hilo, alisema, "Los Angeles imeangamia." Nayo imekwisha. Sijui ni lini. Siwezi kuwaambia.

¹⁹⁴ Sikujua nilisema jambo hilo. Lakini ndugu huyu hapa, naamini ilikuwa ni yeye... La. Mmoja wa akina Mosely, ninaamini, alinikuta huko mitaani kule. Sikujua ilikuwa ni nini mpaka nilipoyarejea. Nilirejea kwenye Maandiko.

Naye Yesu alisema, "Kapernaumu, Kapernaumu, ni mara ngapi... Wewe uliyejikuza, hasa, hata Mbinguni, utashushwa mpaka kuzimu. Kwa kuwa kama miujiza mikubwa iliyokuwa imefanyika kwako, ingelikuwa imefanyika Sodoma,

ungalikuwapo mji huo hata sasa.” Na yapata miaka mia moja na hamsini tangu wakati huo, (Sodoma ulikuwa tayari, ardhini) ndipo Kapernaumu uko ndani ya maji, pia, siku hizi.

¹⁹⁵ Na Roho yeye yule wa Mungu aliyesema mambo haya yote, na kufanya mambo haya yote, Yeye alisema hapo, “Ewe, mji, Kapernaumu, uliyejiita kwa jina la Malaika, Los Angeles, jinsi ulivyojitukuza hata mbinguni! Shina lenyewe na kiti cha Shetani, unaona, umejitukuza.”

¹⁹⁶ Wahubiri, ni makaburi kwao. Watu wazuri huenda kule kisha wanakufa kama panya. Ni maangamizi ya jinsi gani!

¹⁹⁷ “Wewe unayejiita kwa jina la Malaika; kama miujiza hiyo mikubwa ingalifanyika Sodoma, iliyoifanyika kwako, ungalisimama mji huo hata sasa. Lakini saa yako imewadia.”

Ninyi angalieni muone. Kama hautazama, mimi ni nabii wa uongo. Unaona? Huo hapo. Umekaa pale.

¹⁹⁸ Ninakumbuka usiku huo, kabla sijaona jambo hilo, niliona onesho la awali la Bibi-arusi. Nilisimama pale na nikamwona maskini bibi mdogo mzuri, amevalishwa vizuri tu, na kadhalika, akitembea kiaskari namna *hii*. Kulikuwako na Mtu fulani amesimama karibu nami, katika hilo ono. Ndipo nikaona. Wakisema, “Onyesho la awali la Bibi-arusi.” Nikamwona akipita. Walitokea upande *huu*, kisha wakazunguka.

¹⁹⁹ Nami nikalisikia likija; maka—makanisa yakija kutoka upande huu *mwingine*. Hili hapa kanisa la Asia linakuja. Loo, nena kuhusu uchafu! Hili hapa kanisa la Ulaya linakuja. Loo, jamani! Ndipo nikasikia roki ikija, na ilikuwa ni Bi Marekani, kanisa, na hata hakuwa amevaa nguo zo zote. Alikuwa na makaratasi, kama magazeti, kijivu, ameyashikilia mbele zake, akicheza roki; Bibi Marekani, kanisa.

²⁰⁰ Nilisimama hapo katika mbele za Uwepo Wake. Nikawazia, “Ee Mungu, kama mhudumu, kama hilo ndilo jambo zuri sana tungaliweza kufanya? Loo! Loo!” Unajua jinsi unavyojisikia. Kisha nikawazia, “Mungu, nifiche. Laiti ningaliweza kutoroka kutoka hapa. Kama kwa yote ambayo tumefanya, na hayo ndiyo tumezaa, kama hayo ndiyo?”

²⁰¹ Ndipo basi wakati hao wanawake walipopita, wote wakifanya kila namna ya roki na kadhalika, na nywele fupi, na nyuso zilizopakwa rangi. Na wakati walipopita namna hiyo, wakidhaniwa ni bikira kwa Kristo. Na wakati alipopita namna hiyo, niligeuza kichwa changu, mwajua, nikishikilia *hiki* mbele zangu. Ilikuwa—ilikuwa ni aibu sana, nyuma yao. Nao hao hapo, wakienda namna hiyo. Ndipo nikageuza kichwa changu, nikaanza kulia, namna *hiyo*.

²⁰² Nikasema, “Si—singeweza kuvumilia jambo hilo hapo. Yeye akiwa amesimama pale, mimi nikijua ya kwamba mimi, mhudumu wa Kanisa, na hicho ndicho nilichomtolea.”

Nikasema, “Ee, Mungu, siwezi kukiangalia. Hebu na nife. Hebu na—hebu na nitoweke,” na namna hiyo.

²⁰³ Na mara lilipotoka nje, kila mara mmoja wao angetokea, wangeenda mahali fulani, kisha wakatoweka. Nami ningesikia tu sauti yake walipokuwa wanatoweka.

Ndipo nikasikia kitu kama *Twendeni Askari*. Nami nikaangalia, na hapa likaja kundi la wasichana wadogo watakatifu jinsi hasa walivyokuwa, wote wamevalia vizuri, nywele zao zikining’inia chini kabisa mgongoni mwao. Laini, wasafi, wakienda kiaskari namna *hii*, kwa hatua za Injili. Yeye alikuwa ni Neno. Walionekana kama ni mmoja kutoka katika kila taifa. Nilikuwa nikiwaangalia walipokuwa wanapita, na nikawaona wakipita. Badala ya kushuka kwenda chini, walianza kupanda juu.

Nami nikaona mmoja wao akijaribu, wawili ama watatu wao wakijaribu, wakitoka mstarini. Nikapaza sauti. “Rudini kwenye mstari.” Ndipo hilo ono likaniacha. Nami nilikuwa nimesimama katika chumba hiki, nikapasa sauti, “Rudini kwenye mstari.” Mstari, Huo.

²⁰⁴ Sijui, inawezekana imepita tayari? Inawezekana kwamba Bibi-arusi ameitwa tayari? Hilo ndilo tunalopitia leo?

Anapaswa kufinyangwa na kuumbwa kuwa sura ya Kristo, naye Kristo ni Neno. Hilo ndilo jambo pekee. Unaona? Liko Humo ndani, katika Neno. Ni ninii tu. . . Unaona? Haiwezekani kuongeza jambo moja. Haiwezekani mwa—mwanamke awe na mkono mmoja kama wa mwanamume, na mkono huo mwingine wenye wayo kama wa mbwa. Haina budi kuwa ni Neno la Bwana hasa, kama vile Yeye alivyo Neno. Bibi-arusi ni sehemu ya Bwana-arusi. Mwanamke ni sehemu ya mumewe, maana yeye ametolewa kwa mumewe. Hawa alikuwa ni sehemu ya Adamu kutoka ubavuni mwake. Na vivyo hivyo na Bibi-arusi, hatolewi kwa madhehebu, bali anatolewa kutoka kifuni mwa Neno la Mungu la siku hizi.

²⁰⁵ Kunyakuliwa!

Parapanda ya Bwana italia; wafu katika Kristo
watafufuka,
Na kushiriki utukufu wa kufufuka Kwake;
Wakati waliochaguliwa watakapokusanyika
nyumbani mwao ng’ambo ya mbingu.

Majina yaitwapo huko ng’ambo, hebu na sisi sote tujaribu kuwa Kule, enyi marafiki. Mungu awabariki,

²⁰⁶ Limenenwa. Halina budi kutimia. Litatimia. Nanyi nanii wadogo. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Enyi watu, hakuna mtu anayetaka kufa. Hakuna mtu anayetaka ku—kupotea. Hebu niwaambieni. Lo lote mfanyalo. . . Sijali jinsi mnavyohudhuria kanisa vizuri, na jinsi

mlivyo waaminifu kwa kanisa. Hilo ni zuri; sina neno dhidi ya jambo hilo. Mnapaswa kwenda kanisani. Fanyeni hivyo. Endeleeni kwenda kanisani. Lakini, hata iwe nini, tupilieni mbali mapokeo yenu, na msonge mbele mwende moja kwa moja kwa Kristo. Maana, italia moja ya siku hizi, nanyi mtashikwa mkiwa na alama ya mnyama, wala hamtajua ni kitu gani mpaka mtakapokuwa mmechelewa sana. Hiyo ni kweli kabisa.

²⁰⁷ Mungu awabariki. Ninasikitika kuwakawisha. Basi kumbukeni. Nimewaweka kwa muda mrefu sana hapa. Hiyo ni kweli. Na matoleo ambayo mmenitolea . . . Ambayo, sikuwaomba kufanya hivyo, Ndugu. Hiyo ni ninii yangu, hiyo ni heshima. Chukueni hayo na mkalipie hoteli hii o—ovataimu, maana niliwachelewesha. Nilikuwa tu na mambo machache hapa. Nina kurasa kama nane ama kumi zaidi juu ya huko Kunyakuliwa pale, bali kamwe si—sikapata wakati wa kuutoa. Mungu awabariki.

²⁰⁸ Mnampenda Bwana Yesu? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hebu na tusimame kimya tu kwa dakika chache sasa, kimya, kwa uchaji, pia kumbukeni yale niliyosema. Kumbukeni, tuko katika saa za mwisho.

Mataifa yanavunjika; Israeli inainuka;

Ishara ambazo Biblia ilitabiri:

Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekubwa na hofu;

“Rudini, enyi mliotawanyika, makwenu.”

Siku ya ukombozi imekaribia,

Mioyo ya watu inakufa kwa hofu;

Jazweni na Roho, Taa zenu zimesafishwa na ni safi.

Angalieni juu, ukombozi wenu umekaribia.

Mnajua hivyo?

Manabii wa uongo wanadanganya. Kweli ya

Mungu wanaikana.

Tunajua ya kwamba hayo yote ni kweli, sivyo? [Sehemu tupu kwenye kanda-Mh.]

Nampenda, nampenda

Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu

Mtini Kalvari.

²⁰⁹ Ni wangapi wanaompenda kwelikweli. Inua mkono wako. Sasa, ninawatakeni, wakati tukiimba huu tena, peana mikono na mtu aliye karibu nawe. Useme, “Mungu akubariki, msafiri.” Sisi ni wasafiri. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Wasafiri na wageni.

Nampenda,

Namna hiyo, moja kwa moja upande wa pili wa meza.

Nampenda
 Kwani alinipenda kwanza
 Na kununua wokovu wangu
 Mtini Kalvari.

²¹⁰ Unataka kuingia katika Kunyakuliwa? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ni wangapi wanaotaka kuingia katika Kunyakuliwa? Waseme, "Mungu, ninataka nipate kunyakuliwa, kwa moyo wangu wote."

Shikilia Mkono wa Mungu Usiobadilika, mnaujua wimbo huo? Unaujua, dada? *Shikilia Mkono wa Mungu Usiobadilika*. Sijui nini . . . Uko wapi, huo? En-he?

Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
 Jenga matumaini yako kwenye mambo ya
 milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Mnaupenda huo?

Wakati safari yetu imekwisha,
 Kama umekuwa mwaminifu kwa Mungu,
 Makao yako ya utukufuni ni mazuri na yenye
 kung'aa,
 Nafsi yako iliyojaa furaha itayaona!
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
 Jenga matumaini yako juu ya mambo ya milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

Ninawatakeni mwinamishe vichwa vyenu kwa muda kidogo sasa.

Usitamani utajiri usio na maana wa
 ulimwengu huu,
 Unaoza upesi sana,
 Tafuta kupata hazina ya Mbinguni,
 Havitapita kamwe!
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!
 Jenga matumaini yako kwenye mambo ya
 milele,
 Shikilia mkono wa Mungu usiobadilika!

²¹¹ Vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa, na jambo hili likiwa niani mwenu, tukijua ya kwamba tunainamisha vichwa vyetu kuelekea kwenye mavumbi tulimotolewa, siku moja tutarudi, ukijua ya kwamba una nafsi ndani hapo ambayo haina budi kujibu kwa Mungu. Na kama ukijisikia ya kwamba wewe hauko tayari kwa ajili ya huko Kunyakuliwa, kama kungetokea usiku wa leo, na ungetaka kukumbukwa katika maombi, inua tu mkono wako. Hatuna mahali pa kufanya wito wa madhabahuni.

Madhabahu yako iko moyoni mwako, hata hivyo. Inua mkono wako. Mungu akubariki, wewe, wewe. Jamani!

“Ninajisikia siko tayari, Ndugu Branham. Mi—mimi, kweli, ni—ni—ninataka kuwa Mkristo. Nimejaribu kuwa, bali daima kuna kasoro fulani. Ni—ninajua ya kwamba si—siko mahali ninapopaswa kuwa.”

“Nirehemu, Mungu. Ninainua mkono wangu. Nirehemu mimi.”

Sasa, mikono ishirini ama thelathini imeinuliwa, tayari, katika kundi hili dogo. Mengine inainuliwa.

²¹² Mungu mpendwa, Wewe unajua kilicho nyuma ya mkono ule, kule chini ya moyo huo. Ninaomba, Mungu mpendwa. Mimi ninawajibika kwa jambo moja tu, hilo ni, kusema Kweli. Na, Mungu mpendwa, wao wanataka kuokolewa. Wanataka, kweli. Ha—hawataki jambo fulani hili ambalo ni mhemko fulani tu, kujichochea fulani, mfumo fulani wa kimadhehebu, kanuni fulani ya imani, fundisho fulani la sharti ambalo limeongezwa. Wao wanafahamu, Baba, ya kwamba inahitaji Neno safi, lisiloghoshiwa la Mungu. Mengine yote yatapita, hata mbingu na nchi, bali Hilo halitapita. Na kama sisi ni Neno hilo, nchi itapita kutoka chini yetu, bali sisi hatuwezi kupita kamwe, kwa maana sisi ni Neno hilo, Bibi-arusi wa Bwana Arusi.

²¹³ Ninaombea kila mmoja, ya kwamba Wewe utawajalia, Baba, ndilo ombi langu aminifu. Na samahani, Baba, kwa kuwa na wasiwasi mno usiku wa leo, kuruka hapa nimechelewa, na—na kutetemeka, na kusema maneno yaliyokatika na kukatwakatwa. Kwa namna fulani au nyingine, ewe Roho Mtakatifu mkuu, yaunganishe pamoja kwa njia Yako Mwenyewe ya Kiungu, na kuyaingiza katika mioyo ya watu, kutoka moyoni mwangu, na nia na kusudi nililo nalo moyoni mwangu kwa ajili Yako. Utajalia, Bwana? Na uwaokoe hao wanaoweza kuokolewa. Wavute Kwako, Bwana. Na jalia tuwe tayari kwa ajili ya hiyo saa ya kunyakuliwa ambayo imekaribia. Kwa kuwa naomba jambo hilo katika Jina la Yesu. Amina.

Mungu awabariki.

Sasa, mwenyekiti wa—wa mkutano huu.



UNYAKUO SWA65-1204
(The Rapture)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumamosi jioni, tarehe 4 Desemba, 1965, katika Ramada Inn kule Yuma, Arizona, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2007 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org